BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,019,301,493/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#



**Wanawake** 10 walivyong'ara uteuzi mpya wa majaji

UKURASA 3



NANDY HANA UGOMVI NA ZUCHU

UKURASA 20

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Agosti 7, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581030

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


RIPOTI MAALUM

# MAJANGA SHULENI

• **Madarasa** matatu watumia chumba kimoja, vyoo hatarishi... *Endelea ukurasa 4*



Mwalimu wa Mazingira, Afya na Michezo katika Shule ya Msingi Kiboriani wilayani Mpwapwa, akionesha moja ya nyumba zinazotumika kwa makazi ya walimu shuleni hapo wiki iliyopita. **Chini;** nyumba nyingine ya walimu shuleni hapo. **PICHA ZOTE: SANULA ATHANAS**

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### ANUSURIKA KIFO TUHUMA MAPENZI NA MWANAFUNZI

MKAZI wa Mtaa wa Masekelo, Manispaa ya Shinyanga, Charles Kundi (59), amesurika kifo kutoka kwa wananchi baada ya kudaiwa kukutwa nyumbani kwake akifanya mapenzi...

UKURASA WA 3

### WATAALAMU: MAZIWA YA MAMA NI AKILI YA MTOTO

WATAALAMU wa masuala ya lishe wamesema maziwa ya mama humfanya mtoto kuwa na akili na mwenendo mzuri...

## Rais Samia aonya vigogo makusanyo halmashauri

UKURASA 2



## Majaliwa atoa ufafanuzi zuio chakula kuuzwa nje

UKURASA 2

MICHEZO MAYELE: NITAENDELEA KUTETEMA UK.23 | MAONI, KATUNI UK.6



Mkulima wa mboga, Bhoke Mussa, akiendelea na shughuli katika bustani yake, eneo la Kipunguni, jijini Dar es Salaam jana. Bhoke alikabidhiwa matuta 24 na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, ili kujishughulisha na kilimo mboga baada ya kuachana na kazi ya ungariba. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Samia awaonya vigogo mapato ya halmashauri

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameziagiza halmashauri zote nchini kuhakikisha zinakusanya vizuri mapato na kuyawasilisha kwa wakati kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ili kurahisisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alitoa agizo hilo jana wilayani Chunya mkoani Mbeya alipozungumza na wananchi wa wilaya hiyo katika Kata ya Matundasi baada ya kuzindua barabara ya Chunya-Makongolosi yenye urefu wa Km 39.

Alisema kumekuwa na tatizo la baadhi ya halmashauri kujikadiria makusanyo kidogo wakati wa maandalizi ya bajeti ambayo hayaendani na uhalisia wa vyanzo vya mapato kwenye maeneo yao.

Mkuu wa Nchi alisema ili kudhibiti tabia hiyo, amewaagiza mawaziri wawili kupita katika halmashauri zote nchini kuangalia na kutathmini uhalisia wa vyanzo vya mapato na makusanyo yake kwa mwaka.

Mawaziri waliopewa agizo hilo ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba.

"Nimewatuma mawaziri Innocent Bashungwa pamoja na Waziri wa Fedha wapite kwenye halmashauri zote kuangalia vyanzo vya mapato na uhalisia wa ukusanyaji wa mapato, ninajua siyo halmashauri zote zinazojikadiria kukusanya mapato kwa kiwango cha chini.

"Ripoti yao itatusaidia kuboresha ukusanyaji wa mapato kwenye halmashauri zetu, japokuwa mwaka wa fedha uliopita makusanyo yalikuwa vizuri, lakini lazima tufuatilie," alisema.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Nchemba, alisema wapo watendaji wa halmashauri nchini ambao wamekuwa wakipatiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi lakini mpaka mwaka wa fedha unaisha wanakuwa hawajatekeleza miradi ya aina yoyote.

Alisema baada ya kutotekeleza miradi hiyo, watendaji hao wamekuwa wakirejesha fedha hizo wizarani, hali ambayo alisema inawanyima wananchi fursa wanazokuwa wameandaliwa na serikali yao.

"Mheshimiwa Rais, baada ya kukamilika kwa ripoti hii, watendaji hawa watapitiwa na fagio la chuma, hatuwezi kuwavumilia wakati wanawakwamisha wananchi kupata huduma," alionya.

Katika hatua nyingine, Rais Samia amewataka viongozi wa serikali kushirikiana na wananchi kulinda miundombinu ya barabara, ikiwamo kuzuia shughuli za kibinadamu kwenye hifadhi za barabara na madaraja ili kuipunguzia serikali gharama za ukarabati.

Alisema serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kujenga miundombinu hiyo lakini baadhi ya watu kuiharibu kwa makusudi huku akitolea mfano wilayani Chunya ambako wananchi wanachimba madini kwenye hifadhi za barabara na kuchimba mchanga chini ya madaraja.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi wa barabara hiyo ya Chunya-Makongolosi, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema ni mwendelezo wa ujenzi wa barabara ya Mbeya-Singida-Tabora kwa kiwango cha lami na kwamba kwa baada ya kukamilisha kipande hicho, wanakusudia kuanza kipande cha Makongolosi-Lupatingatinga.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Bashungwa, alimwagiza Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kufanya tathimini ya barabara ya Matundasi-Itumbi yenye urefu wa Km 13 ili ijengwe kwa kiwango kinachostahili.

Rais Samia anaendelea na ziara mkoani Mbeya ambapo leo anaratajiwa kuwa wilaya za Rungwe na Kyela kabla ya kufunga maonyesho ya wakulima (Nanenane) na kuhitimisha katika Wilaya ya Mbarali.

## Anusurika kifo tuhuma mapenzi na mwanafunzi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKAZI wa Mtaa wa Masekelo, Manispaa ya Shinyanga, Charles Kundi (59), amesurika kifo kutoka kwa wananchi baada ya kudaiwa kukutwa nyumbani kwake akifanya mapenzi na mwanafuzi wa darasa la sita (jina linahifadhiwa).

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Leonard Nyandahu, alikiri kutokea kwa tukio hilo juzi jioni na sasa wanamshikilia mtuhumiwa kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Masekelo, Elias Mminda, alidai alikuwa na taarifa za mzee huyo kujihusisha kimapenzi na wanafunzi muda mrefu lakini walishindwa kumkamata kutokana na kukosa ushahidi.

Alidai kuwa siku aliyokamatwa, alikutwa anapigwa na wananchi ndipo alipowazuia na kumpeleka polisi.

"Taarifa za mzee huyu kufanya michezo michafu kwa wanafunzi ninazo tangu siku nyingi, na nyumbani kwake huwa anaishi peke yake na baada ya kumhoji mwanafunzi huyu, alitueleza kuwa amekuwa akifanya ngono na mzee huyo siku nyingi," alidai.

Mminda alitumia fursa hiyo kuwaonya watu wazima kuacha tabia ya kufanya ngono na wanafunzi kwa kuwa tukio hilo siyo la kwanza kutokea maeneo hayo.

"Tukio kama hili lilitokea Mei 6 mwaka huu ambapo walikamatwa wanaume wawili akiwamo baba mwenye nyumba kwa tuhuma za kumlawiti mwanafunzi wa darasa la sita," alikumbusha.

Mkazi wa eneo hilo ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini, alisema wamechoshwa na vitendo hivyo vya watu wazima kushiriki mapenzi na wanafunzi na kuwaharibia ndoto zao.

# Majaliwa atoa ufafanuzi zuio chakula kuuzwa nje

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa amesema serikali 'imesitisha kidogo' uuzaji wa chakula nje ya nchi kutokana na uwezekano wa kutokea baa la njaa nchini.

Alitoa ufafanuzi huo juzi alipozungumza na wananchi wa Tarafa ya Ikungi baada ya kukagua na kuweka jiwe la msingi mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Ikungi unaotarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. bilioni 1.9.

Majaliwa alitoa ufafanuzi wa suala hilo baada ya Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Singida, Martha Gwau, kuomba msaada kwa ajili ya wananchi wa Wilaya ya Ikungi ambao wanakabiliwa na upungufu wa chakula. "Wale ambao mnatamani kuuza nje, muungane na sisi kwenye mtizamo huu wa mashaka mashaka, kwamba lazima tuanze kukiangalia chakula chetu tusije tukaanza kuuza nje sababu tu wakulima mna hamu ya kuuza nje, tusije tukafa kwa njaa," Waziri Mkuu alisema.

Majaliwa alisema hata mataifa ambayo yalikuwa yanakuja kuchukua chakula, serikali imezuia kwanza kuangalia kama ikifika Oktoba mwaka huu mvua itaanza kunyesha ndipo itaangalia kuuza chakula nje kama kitakuwapo.

"Chakula tulichonacho wacha tukihifadhi kidogo, tugawane gawane hadi mvua zianze na kama zitaanza kama tutakuwa nacho tutaruhusu muuze," alisema.

Majaliwa alisema serikali imeruhusu Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kununua chakula kuliko kumuuzia mtu wa nje. "Tumeruhusu NFRA anunue alete kwenye ghala, tukipata shida tuchukue kwenye ghala maana hatuwezi kuchukua tena nje kule ambako tumekiuza," alisema.

Kuhusu ujenzi wa Mji mpya wa Ikungi unaojengwa eneo la Unyahati katika Kijiji cha Muungano barabara kuu ya Singida-Dodoma, aliwasihi wananchi wasianze kukwamisha mradi huo kutokana na kudai masuala ya fidia.

"Tuna sheria hata kama una hati ya eneo lako usipoliendeleza kwa miezi 36, serikali inachukua ardhi yake na kupanga matumizi mengine," alisema.

Alisema zipo taarifa kuwa baadhi ya watu wanang'ang'ania fidia wakati hawajawahi hata kulima maeneo hayo na kusahau kuwa ipo sheria ya ardhi inayoelezea miezi 36. Majaliwa aliwataka wananchi kuwa wazalendo na kuitaka halmashauri ianze kuuza viwanja katika eneo la mji mpya unapojengwa kwa gharama nafuu ambazo hata wananchi wa kawaida watazimudu.



Ofisa Mtendaji Kata ya Kunduchi, Abel Silaa,(kushoto) akizungumza na wazazi na wanafunzi 17 waliohitimu mafunzo ya kushona yaliyotolewa na Kampuni ya Binti Afrika, mafunzo ya miezi mitani (5) ya kushona nguo za aina mbalimbali kupitia Taasisi ya Binti Foundation kupitia Kampuni ya Binti Afrika inayoongozwa na Mkurugenzi Mkuu, Johari Sadiq ambaye mpaka wanafanya Mahafali ya 4 juzi wamefanikiwa kuwafundisha wanafunzi 80. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wanawake wang'ara uteuzi mpya wa Rais

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewateua maofisa 22 kuwa majaji wa Mahakama Kuu, huku wateule 10 wakiwa wanawake, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi yake ya kulipa nafasi za uongozi kundi hilo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rai, Ikulu, Zuhura Yunus, wanawake waliopo kwenye uteuzi huo ni Happiness Ndesamburo ambaye kabla ya kuteuliwa alikuwa ni Naibu Msajili wa Mahakama.

Wengine ni Victoria Nongwa, aliyekuwa Naibu Msajili wa Mahakama, Ruth Massam aliyekuwa Naibu Msajili wa Mahakama na Gladys Barthy, ambaye alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama.

Wateule wengine wanawake ni: Fatma Khalfan ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Kamishna Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Monica Otaru aliyekuwa Mkurugenzi Msaidizi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na Marlin Komba ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Mkurugenzi wa Sheria Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Wengine ni Dk. Mwajuma Juma, Mhadhiri Msaidizi, Chuo Kikuu cha Mzumbe; Asina Omani, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Aisha Bade, Wakili wa Kujitegemea. Wateule wengine ni Kevin Mhina ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Msajili wa Mahakama ya Rufani; Gabriel Malata, Wakili Mkuu wa Serikali na Adrian Kilimi aliyekuwa Naibu Msajili Mahakama.

Pia wamo Obadia Bwegoge aliyekuwa Naibu Msajili wa Mahakama na Godfrey Isaya aliyekuwa Naibu Msajili wa Mahakama.

Rais pia amemteua Haji Suleiman Haji ambaye ni Mwendesha Mashtaka Mfawidhi Mahakama Kuu, Zanzibar, Abubakar Mrisha, Wakili wa Serikali na Lusungu Hongoli, Wakili Mkuu wa Serikali Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Taarifa hiyo iliwataja wengine kuwa ni Kamana Stanley ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi (TAMISEMI), Hamidu Mwanga, Mkurugenzi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Dk. Cleophas Morris, Mhadhiri wa Chuo Kikuu Dar es Salaam na Mussa Pomo ambaye ni Wakili wa Kujitegemea. Tarehe ya uapisho wa majaji wateule itatangazwa baadaye.

# Wataalamu: Maziwa ya mama ndiyo akili ya mtoto

**Na Steven William,** MUHEZA

WATAALAMU wa masuala ya lishe wamesema maziwa ya mama humfanya mtoto kuwa na akili na mwenendo mzuri katika kujifunza mazingira na uelewa mpya.

Ofisa Lishe Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Emmanuela Lawrence, alibainisha hayo jana wakati wa uzinduzi wa maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji uliofanyika kwenye Kituo cha Afya Ubwari, mgeni rasmi akiwa Diwani wa Genge, Moses Kisiki.

Alisema utafiti unaonyesha maziwa ya mama humfanya mtoto kuwa na akili na mwenendo mzuri katika kujifunza mazingira na uelewa mpya.

Lawrence alisema unyonyeshaji wa maziwa ya mama ni muhimu kutokana na faida ambazo humpatia mtoto virutubisho vyote anavyohitaji kwa uwiano sahihi wa ukuaji na maendeleo yake.

Alisema maziwa ya mama pia humpatia mtoto kinga dhidi ya maradhi mbalimbali kama kuharisha na magonjwa ya mfumo wa hewa.

Ofisa Lishe huyo alisema maziwa ya mama ni safi na salama, hupatikana muda wote katika joto sahihi na yanakaa saa nane bila kuharibika katika joto la kawaida.

Lawrence alisema pamoja na juhudi zinazofanywa kwa lengo la kujenga mazingira wezeshi kwa wanawake wanaonyonyesha, bado kuna vikwazo mbalimbali vinavyochangia kupunguza kasi ya unyonyeshaji katika jamii.

Alisema wazazi wengi mara nyingi wanazingatia zaidi masuala ya kujifungua kuliko mambo muhimu baada ya kujifungua kama vile kunyonyesha, huku kukiwa na kikwazo cha uhaba wa wafanyakazi na watoa huduma za afya wanaopaswa kutoa elimu ili wanawake wajue umuhimu wa kunyonyesha.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Frola Kessy, alisema maziwa ya mama yana umuhimu mkubwa kwa mtoto,m akiwahimiza wazazi watimize wajibu wao kwa kuepuka kuwaachisha mapema ama kuwanunulia maziwa ya wanyama watoto wao.

Diwani wa Genge, Kisiki, alisema kinamama lazima wajenge utamaduni wa kunyoyesha watoto huku akiagiza watoa huduma za afya kutoa elimu kwa wazazi ili wajue wajibu wa kuwanyonyesha watoto wao.

# CCM yaagiza MSD ipeleke dawa ilikositisha huduma

**Na Mary Geofrey,** MWANGA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimeiagiza Bohari ya Dawa (MSD) kuendelea kupeleka dawa kwenye Zahanati ya Vuchama iliyoko Kata ya Mwanilo, ambako bohari lisitisha kupeleka huduma kutokana na kudaiwa Sh. milioni 104.

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, amesema tatizo la deni la dawa walilonalo siyo sababu kwa MSD kusitisha kupeleka dawa katika zahanati hiyo kwa kuwa wananchi wanahitaji kuendelea kupata huduma.

Chongolo alitoa agizo hilo muda mfupi baada ya kupokea maelezo kuhusu kero ya zahanati hiyo kukosa dawa kutokana na kudaiwa, alipozungumza na wana-CCM katika Kijiji cha Vuchamangofi akiwa katika ziara ya kukagua utekelezaji wa ilani ya chama, miradi ya maendeleo na kuhimiza ushiriki wa Sensa ya Watu na Makazi.

Diwani wa Mwanilo, Baraka Maridona, alimweleza Katibu Mkuu kuwa zahanati inadaiwa Sh. milioni 104 na ndiyo sababu MSD kuacha kusambaza dawa.

"Nimesikitishwa kwa kweli kusikia eti dawa haziji kwa sababu kuna deni, hii siyo sawa, lazima tujue kama kuna changamoto, tutafute namna ya kuitatua lakini tusikatishe huduma kwa wananchi," aliagiza Chongolo.

Alisema wapo wananchi ambao wana bima ya matibabu na wanazilipia lakini wakienda zahanati kutibiwa, wanakosa dawa, jambo hilo siyo sawa na hakubaliki.

"Ninajua pamoja na kufikiri kuwa mna deni la dawa, fedha hutolewa na serikali za kununulia dawa katika kila zahanati kwenda MSD kwa ajili ya kusambaza dawa chini, mimi nakwenda kukaa na wataalamu waniambie zahanati zote zilizopo Ugweno zinadaiwa shilingi ngapi na kama nao wanadai au ninyi mnadai kule hilo deni lifutwe ili kuendelea kuletewa dawa.

"Tumeahidi kulinda afya za wananchi, mwananchi mmoja akipotea ni hasara kwa nchi na hatuwezi kutuhusu mwananchi apoteze maisha eti kwa sababu anadaiwa hela ya dawa wakati ugonjwa unatibika," alisema.

Alisema dawa zinahitajika na haiwezekani chama kikae kimya kwenye jambo hilo ambalo siyo mpango wa serikali.

Sambamba na hilo, aliwakumbusha wananchi wa kijiji hicho wanaohitaji kuwekewa umeme gharama zake ni Sh. 27,000 kwa vijijini na siyo vinginevyo kama ambavyo wamekuwa wakidanganywa.

"Msikubali kutozwa zaidi ya Sh. 27,000, kwa sasa umeme siyo hanasa, kila mtu anatakiwa kupata huduma hii kwa gharama ya chini kwa sababu serikali imeamua kutoa huduma hii maeneo yote nchini," alisisitiza.

RIPOTI MAALUM

## KIBORIANI

# Shule yenye mazingira hatarishi kwa wanafunzi, walimu na elimu

## ■Vyoo chakavu, baridi limetawala sakafu
## ■Madarasa matatu ndani ya chumba kimoja

**Na Sanula Athanas**

ILIKUWA majira ya saa tano asubuhi Alhamisi ya juma lililopita, Nipashe ilipozuru kikazi katika Kijiji cha Kiboriani, husuan kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Kiboriani wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma.

Licha ya kupata sura moja ya ukarimu wa ukaribisho kutoka kwa wenyeji shuleni, mrejesho ulitekwa zaidi na ugeni dhidi ya mandhari yaliyoshuhudiwa. Mazingira yamezungukwa na ukungu, baridi la hali ya juu kuliko uhalisia ulioko wilayani humo.

Ilipo shule hiyo ni umbali wa kilomita 13 kaskazini mwa Mji wa Mpwapwa lakini uhalisia wa safari yake kutokana na mizunguko ya mlima, unaunda kilomita 21 kutoka mjini. Utofauti huo wa ziada unatokana na safari ya kuupanda mlima huo wa Kiboriani wenye urefu wa mita 1,846. Kwa lugha rahisi, ni kilomita mbili kasoro kutoka usawa wa bahari.

Wenyeji wanaeleza kwamba kwa kadri ya ukakamavu wao, ni mwendo wa safari ya takriban saa tatu kwa miguu kuifikia shule hiyo unapotoka mjini Mpwapwa.

Kwa mujibu wa wenyeji waliozungumza na Nipashe kijijini Kiboriani, safari hiyo kwa kukodi pikipiki bei yake ni Sh. 15,000 kwa sasa, huku wakisisitiza umahiri wa safari hiyo ni kwa baadhi ya waendesha pikipiki na siyo wote wanaoimudu.

Mbali na mshangao huo wa kimazingira, butwaa lingine liko katika tofauti ya uhalisia wa shule hiyo - ukuta wa madarasa si wa matofali, bali umejengwa kwa udongo staili ile ile ya nyumba za vijijini, juu pameezekwa kwa mabati ambayo nayo yako katika hali mbaya ya uchakavu.

Hali kadhalika, idadi ya vyumba vya madarasa ni ndogo, vipo vinne tu, lakini hapo Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Satiel Kasanda (33), anawafumbua macho wageni waliotekwa na mshangao, akidokeza kuna chumba kingine kidogo hapo katikati ya vyumba vya madarasa ambacho ndicho ofisi yake.

Ndani ya simulizi hizo za kufumbuliwa macho na masikio, Mwalimu Mkuu Kasanda anasema hiyo ni shule inayomilikiwa na serikali na ilianza kutoa huduma mwaka 1979, kwa lugha nyepesi, ina umri wa miaka 43.

**MASOMO YANAENDAJE?**

Mshangao huo ndiyo ulioibua maswali zaidi ya kiuandishi wa habari kutaka kujua jinsi masomo yanavyokwenda. Hapo Mwalimu Mkuu Kasanda ana ufafanuzi, akitamka:

"Kama unavyoona hali halisi hapa shuleni, tuna wanafunzi 420 (wasichana 227) ambao kukaa na kusoma kwao darasani ni shida. Walimu tumebuni mbinu ya kuwapanga 'kushoto-kulia', yaani kwenye chumba kimoja cha darasa, kwa mfano kile pale (anaonesha kwa ishara ya mkono), la tano wanaketi kushoto na la sita wanaketi upande wa kulia ndani ya chumba hicho hicho.

"Mwalimu akiingia kufundisha darasa la sita, basi inabidi wanafunzi wa darasa la tano wanyamaze kimya. Maana yake ni kwamba mwalimu aliyekuwa na kipindi kwa wanafunzi wa darasa la tano, inabidi asifundishe muda huo.

"Mbaya zaidi, humo ndani ya darasa madawati hayatoshi. Wanafunzi wa darasa la tatu hadi la saba wanalazimika kuketi watano hadi sita kwenye dawati moja.

"Wale wa madarasa ya chini kwa maana ya wanafunzi wa darasa la awali hadi la pili, wanalazimika kuketi sakafuni. Hakuna madawati kwenye chumba chao. Hii ndiyo hali halisi hapa shuleni, wanafunzi wanalazimika kusoma katika vyumba hivi vinne vilivyopo kwa mbinu hizi."

Kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, kila chumba cha darasa kinapaswa kutumiwa na wastani wa wanafunzi 45. Hapo ina maana kwamba wanafunzi 420 wa Shule ya Msingi Kiboriani yenye vyumba vinne pekee vya madarasa kwa sasa, wanapaswa kuwa na vyumba tisa (9).

**BAA LA VYOO**

Huo ni mtihani wa darasani. Idadi hiyo ya wanafunzi wapatao 420 kutoka Shule ya Msingi Kiboriani, wote wa kijiji hicho, wana shida nyingine ya pili inayohusu vyoo, kwamba viko katika hali mbaya inayokinzana na uhalisia wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na maelekezo mbalimbali, yakiwamo mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya Aprili 2017, ambaye pia alifunga safari ya kwenda kupata ushuhuda wa kilichopo shuleni hapo miaka mitano iliyopita.

Kimsingi, idadi ya matundu ya choo shuleni ni manne, kwa maana mawili kwa wavulana na mawili kwa ajili ya dada zao. Vivyo hivyo, walimu wao kujumlisha na mkuu wao, wako watano, wana matundu mawili ya choo.

Nipashe ilishuhudia hali mbaya ya matundu hayo ya vyoo, uchakavu wa sakafu yake na kwa macho kuna viashiria vya kuporomoka wakati wowote. Pia kuna matobo yanayoonyesha kila kilichopo kwenye shimo la choo na majimaji yaliyotuama kwenye sakafu.

Kingine kinachokinzana na kanuni za afya na usalama, ni hali ya kuta zenyewe zilizojengwa kwa udongo, zina kiashiria cha kubomoka, vyoo havina milango bali vimejengewa kona inayomsitiri aliyeko ndani, lakini vina paa la bati lililochakaa.

Akitoa ufafanuzi kwa Nipashe kuhusu huduma ya choo shuleni hapo, Ofisa Mtendaji wa Kijiji, Ramadhan Mfundo, anasema tayari kuna majanga kwenye vyoo hivyo, kwamba mwaka jana mwanafunzi wa darasa la sita alitumbukia, lakini binti huyo akaokolewa kwa msaada wa wanakijiji na walimu baada ya kufikiwa na mbiu ya haraka.

Mwalimu wa Mazingira, Afya na Michezo shuleni hapo, Mussa Ahmad, anasema hatua za tahadhari walizochukua kwa kiwango cha uwezo wao, wameweka utaratibu wanafunzi wadogo hasa kuanzia darasa la awali hadi la pili, wanapokwenda chooni, ni sharti wasindikizwe na ama dada au kaka zao wa madarasa ya juu kusimamia usalama wao.

Uchunguzi zaidi wa Nipashe umebaini kwamba mnamo mwaka 2020, Ofisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya ya Mpwapwa alitaka kuifunga shule hiyo kutokana na uchakavu wa miundombinu ya vyoo alioubaini.



Mwalimu wa Mazingira, Afya na Michezo katika Shule ya Msingi Kiboriani, Mussa Ahmad, akionyesha moja ya madarasa ya shule hiyo.

Nipashe imebaini ofisa huyo alitoa hadhari kuwa hali ya vyoo katika shule hiyo ni hatari kwa usalama wa wanafunzi, angalizo ambalo mwaka jana lilidhihirika kwenye tukio la mwanafunzi wa darasa la sita kutumbukia chooni.

"Dosari hii imepelekea wakati mwingine wanafunzi kujisaidia vichakani na wengine hurudi nyumbani kwenda kujisaidia wakati wa masomo. Miundombinu ya vyoo iliyopo imechakaa, ujenzi wa vyoo vipya unahitajika," inasomeka sehemu ya Taarifa ya Ofisa Afya wa Wilaya ya Mpwapwa ya mwaka 2020 iliyomsukuma Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya kutaka kuifunga shule hiyo.

Baadhi ya mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hiyo ni vyoo viongezwe kwa kuwa vilivyopo ni vichache na havina ubora, huku kukiwa na angalizo kwamba jambo hilo lisipofanyiwa kazi mapema, uamuzi wa kuifunga shule hiyo uchukuliwe katika ukaguzi unaofuata.

Licha ya kutolewa kwa angalizo hilo miaka miwili iliyopita, hadi sasa wanafunzi wa Shule ya Msingi Kiboriani wanaendelea kutumia matundu manne ya choo kilichochakaa.

Kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, kiwango kinachotakiwa ni kila tundu moja la choo kutumiwa na wanafunzi 20 wa kike na 25 wa kiume.

Kwa mantiki hiyo, Shule ya Msingi Kiboriani yenye wanafunzi 420, ina uhitaji wa matundu 11 kwa ajili ya wasichana 227 waliopo na manane kwa ajili ya wavulana 193 waliopo. Hivyo, jumla ya matundu ya vyoo yanayohitajika shuleni hapo ni 19.

**ITAENDELEA KESHO**


Choo cha wanafunzi wa Shule ya Msingi Kiboriani. **PICHA ZOTE: SANULA ATHANAS**

HABARI KITAIFA

# TRA yatoa msaada kwa hospitali Polisi

**Na Baraka Jamali,** MTWARA

MAMLAKA ya Mapato (TRA) imekabidhi msaada wa vitanda 24 vyenye thamani ya Sh. milioni 12.7 katika Hospitali ya Polisi iliyoko Manispaa ya Mtwara Mikindani ili kuunga mkono jitihada za ujenzi wa wodi hospitalini huko.

Kwenye hafla ya kukabidhi msaada huo juzi, Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo, alisema msaada huo umelenga kuendeleza kutoa huduma kwa wananchi.

"Tuna jukumu la kurudisha kwa jamii kwani dhamira yetu siyo kukusanya mapato tu bali pia kutoa huduma na tumeguswa na juhudi hizi ambazo zinafanywa na Jeshi la Polisi mkoani Mtwara, ndiyo maana tukaona na sisi tuwe sehemu ya kutoa chochote.

"Tunatoa vitanda 24 ambavyo vina thamani ya Sh. milioni 12.7 na tunaamini vitasaidia katika wodi hizi na kutokana na huduma bora mnazozitoa kwa jamii ambayo inawazunguka," alisema.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Kamishna Msaadizi Nicodemus Katembo, alisema mradi huo wanaoutekeleza mpaka sasa umeghalimu Sh. milioni 175.6 na utakapokamilika utagharimu Sh. milioni 185.85.

Alitoa shukrani kwa TRA kutokana na msaada huo ambao utasaidia wananchi watakaotumia jengo hilo, akibainisha kuwa kituo kilichopo sasa kinatoa huduma kwa watu zaidi ya 5,000 kwa miezi mitatu.

"Ujenzi wa jengo hili umefikia asilimia 98 na tayari tumetumia Sh. 175.600,000, leo (juzi) TRA mmetuona na kutusaidia vitanda hivi, tunawashukuru sana na tunaahidi tutaendelea kutoa huduma iliyo bora kwa jamii yetu inayotuzunguka na ukiangalia huduma kila miezi mitatu ya wagonjwa 5,000 tunawahudumia," alibainisha.

Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dustan Kyobya, alilipongeza jeshi hilo kwa huduma linazozitoa ikiwa ni pamoja na kuhudumia idadi kubwa ya wagonjwa katika kituo chake.

"Ninawapongeza kwa huduma mnazozitoa kwa wananchi na jeshi hili limekuwa msaada mkubwa kwa wagonjwa ambao wanapatiwa huduma hapa.

"Pia niwapongeze TRA kwa mchango huu wa vitanda ambao utatusaidia sana," Mkuu wa Wilaya huyo alisifu na kubainisha kuwa jeshi hilo limejikita kutoa huduma kwa wananchi, jambo ambalo ni la kupongezwa na jamii.

Baadhi ya wananchi waliohudhuria hafla hiyo, wakiwamo Juma Nanowa na Zuhura Lazima, kwa nyakati tofauti walitoa shukrani zao kwa jeshi hilo kwa kuwa na kituo kinachowapa huduma za afya pasina ubaguzi.




Spika wa Bunge, Dk Tulia Ackson (kulia) akipata maelezo kuhusu Bima ya Kilimo pamoja na mifugo alipotembelea banda la Shirika la Bima la Taifa kwenye maonyesho ya wakulima Nanenane katika Uwanja vya John Mwakangale, jijini Mbeya mwishoni mwa wiki, akiwa ameongozana na Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde (wa tatu kulia) na (wa pili kulia) Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Simon Simalenga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa awaweka kitanzini watumishi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa amewaagiza wakuu wa wilaya kuhakikisha wanasimamia watumishi wote katika halmashauri za Mkoa wa Singida ambao walikusanya fedha za mapato lakini hawakuzipeleka benki, wazirudishe haraka.

Alitoa agizo hilo jana kwenye kikao cha majumuisho ya ziara yake ya siku mbili mkoani hapa wakati akizungumza na watumishi wa Halmashauri za Wilaya ya Singida, Ikungi na Manispaa ya Singida.

Alisema kumekuwa na tatizo kubwa kwenye halmashauri nyingi nchini katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ambapo baadhi ya watumishi wanapokusanya fedha, haziingizwi kwenye mfumo wa serikali, jambo ambalo limekuwa kero kubwa.

"Wakuu wa wilaya hakikisheni watumishi wanaodaiwa fedha wazirudishe haraka. Iramba, Manyoni na hata Ilongero (Halmashauri ya Wilaya ya Singida) nimepewa orodha ya watumishi ambao wanadaiwa fedha za makusanyo," alisema.

Majaliwa alisema Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza suala la ukusanyaji wa mapato na hata wakati anawaapisha wakuu wa mikoa hivi karibuni, alisisitiza jambo hilo lakini bado kuna baadhi ya watumishi wa umma wamegeuka kuwa wabadhirifu.

Alisema ujanja unaofanywa na baadhi ya watumishi kufuja fedha za makusanyo ni wanapokusanya fedha hasa wanapobaini ni nyingi, wanazima mashine ili zisiingie kwenye mfumo wa serikali.

Waziri Mkuu aliwataka watumishi kuacha urasimu katika utendaji wa kazi kwa kuwa mambo hayo ndiyo yanakaribisha vitendo vya rushwa nchini.

Kuhusu idara za ununuzi, Majaliwa alisema limekuwa ni tatizo kubwa kiutendaji kutokana na idara hizo kuweka makadirio makubwa ya bei za vifaa vya ujenzi kwenye miradi hususan inayotumia 'force account'.

Aliongeza kuwa kwenye halmashauri kumekuwa na tatizo kubwa la usimamizi wa miradi inayotekelezwa na kwamba kuna haja watumishi kuhakikisha suala hilo linapewa msukumo. Majaliwa pia alizitaka halmashauri kuratibu vizuri suala la wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga, ili wapewe maeneo ya kufanyia biashara zao bila usumbufu.

Awali, Waziri Mkuu aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Singida linalojengwa Ilongero katika Kijiji cha Mwahango kwa thamani ya Sh. bilioni 2.7.

Akiwa huko, Majaliwa alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Ester Chaula, kuisimamia idara ya ununuzi ili ujenzi wa jengo hilo ukamilike na kuanza kutumika.

"Nimeridhishwa na ujenzi unavyoendelea, DED (Mkurugenzi wa Halmashauri) isimamie idara ya ununuzi, wasikuvuruge, mkandarasi alipwe fedha zake, " alisema.

Akiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Singida inayojengwa kwa Sh. bilioni 19.5, Waziri Mkuu, alisema ujenzi wa hospitali hiyo utakuwa mkombozi mkubwa kwa wananchi wa mkoa huu na mikoa jirani.

# Wananchi walia na tembo kuvamia makazi na mazao

**Na Mary Geofrey,** MWANGA

WANANCHI wa Vuchamangofi, tarafa ya Ugweno wilayani Mwanga mkoani Kilimanjaro wamelalamika tembo kuvamia makazi na mashamba na kuharibu mazao yao.

Diwani wa Vuchamangofi, Baraka Maradona, aliwasilisha kilio cha wenyeji kwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, jana baada ya kuwasili eneo hilo kuzungumza na wanachama na wananchi katika mwendelezo wa ziara yake mkoani humo ya kukagua utekelezaji wa ilani, miradi ya maendeleo na kuhimiza ushiriki wa Sensa ya Watu na Makazi.

Alisema tembo wamekuwa wakiingia kwenye makazi ya watu na hivi karibuni walimkanyanga mkazi wa eneo hilo na kupoteza maisha.

"Mheshimiwa Katibu Mkuu, tunaomba utusaidie tembo wamemaliza mazao yetu mashambani na kusababisha tukose chakula cha kutosha kwenye msimu huu, tunaomba mtusaidie mamlaka zije ziwadhibiti," alisema.

Chongolo, akijibu hoja hiyo, alisema tayari amezungumza na Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo imeanza kujenga kibanda cha askari wa nyamapori ambao wataletwa kwa ajili ya kuwadhibiti wasiingie kwenye makazi na kuvamia mazao.

"Ninajua tembo wamekuwa changamoto kwenye eneo hili, niwape pole kwa sababu wameathiri maisha ya baadhi yenu wananchi na hivi karibuni tumepoteza ndugu yetu Yonael Mzama kwa kukanyagwa na tembo, niwape pole sana kwa tukio hilo na mengine yanayotokana na madhila ya tembo," alisema.

Chongolo alisema Mkoa wa Simiyu ulikuwa na shida hiyo lakini imefanyiwa kazi baada ya kukubaliana na wizara husika kuweka askari katika maeneo yote yenye tatizo hilo.

Aliwahikikishia wananchi hao kuwa ataisisitiza wizara kupeleka walinzi kwenye eneo hilo ili kudhibiti uharibifu wa wanyama hao.

"Hatuwezi kuona watu wanalima zao kujitafutia chakula halafu wanakuja tembo kusaidia kuvuna, wanamaliza jasho la wananchi wa eneo hili hii haikubaliki kabisa," alisema Chongolo.

Alisema kama viongozi, lazima waratibu na kusimamia jambo hilo ili tembo hao wasilete madhara makubwa kwa wananchi na maeneo mengine.

Sambamba na hilo Chongolo aliagiza Wakala wa Barabara (TANROADS) kuwakata fedha makandarasi wanaochelewesha miradi ili kujenga nidhamu ya uwajibikaji.

Chongolo alitoa hilo wakati akikagua barabara ya Mwanga, Kikweni hadi Vuchama yenye urefu wa Km 29 inayoendelea kujengwa na kuagiza mkandarasi kukatwa fedha kutokana na kuchelewesha kazi hiyo.

Aliagiza fedha atakazokatwa, zitumike kuongeza ujenzi wa kipande kingine ili kuendelea kukamilisha kazi inayoendelea.

Awali, Meneja wa TANROADS Mkoa wa Kilimanjaro, Motta Kyando, alisema ujenzi huo umegharimu Sh. milioni 960 na lengo la mradi huo ni kukamilika Agosti 8 mwaka huu lakini bado kazi kubwa haijafanyika.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua ya serikali kuzuia uuzaji chakula nje mwafaka

**WAZIRI** Mkuu Kassim Majaliwa akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Singida, alitoa ufafanuzi kuhusu uamuzi wa serikali kuzuia uuzaji chakula nje ya nchi huku akitanabahisha kwamba ni kutokana na tishio la njaa linaloikabili Tanzania.

Hatua hiyo ya serikali inatokana na uhaba wa mavuno katika msimu wa kilimo uliopita kutokana na kutokunyesha kwa mvua ya uhakika kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Katika ufafanuzi huo, Waziri Mkuu aliweka bayana kwamba mpango huo hauna lengo la kuwaumiza wafanyabiashara waliopata soko nje ya nchi bali ni kuchukua tahadhari ya kuwapo kwa ukosefu wa chakula.

Ni kweli kwamba katika msimu uliopita wa kilimo wa mwaka 2021/22, mvua haikunyesha kwa wingi jambo ambalo lilisababisha baadhi ya maeneo mazao kunyauka yakiwa katika hatua ya kubeba mahindi au palizi.

Katika mkoa wa Iringa, kwa mfano, maeneo mengi mazao yalinyauka yakiwa katika hatua mbalimbali, hali ambayo imeonyesha wazi kuwa kuna uwezekano wa kuwapo kwa uhaba wa chakula. Hata wale waliobahatika kuvuna, hawakupata mazao ya kutosha kwa ajili ya biashara bali ni kiasi cha kujikimu tu.

Aidha, Majaliwa katika ufafanuzi huo alisema alitoa rai kwa wafanyabiashara na wakulima kuiunga mkono serikali juu ya hatua iliyochukua kwa kuwa ina nia nzuri ya kuwa na akiba ya chakula badala ya kusafirisha nje na baadaye nchi kuagiza kwa kutumia fedha za kigeni.

Pamoja na kutangaza hivyo, Waziri Mkuu aliweka bayana kwamba uamuzi huo wa serikali si wa kudumu bali ni wa muda hadi Oktoba ili kuangalia hali halisi ya akiba na baada ya kuanza kwa mvua za vuli ambazo huwa mahususi kwa ajili ya kupanda mazao mapya.

Kadhalika, alisema serikali haijazuia wafanyabiashara na wakulima kuuza mazao yao bali imefungua milango kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kununua kwa ajili ya kuweka akiba kwa ajili ya tahadhari pindi utakapotokea upungufu wa chakula katika baadhi ya maeneo nchini.


Kwa ujumla, hatua hiyo ya serikali imechukuliwa kwa wakati mwafaka kutokana na ukweli kwamba kuna uwezekano wa nchi kukumbwa na baa la njaa. Hiyo ni kutokana na hali ya mvua kutokuwa ya kuridhisha katika msimu wa kilimo uliopita.

Serikali, kwa kufanya hivyo, imefanya jambo la busara na imeonyesha dhahiri kwamba imetambua tatizo lililopo na kuchukua hatua. Serikali kama mzazi ndani ya familia, imechukua tahadhari kwa ajili ya kuwalinda wananchi wake dhidi ya majanga yatakayotokana na upungufu wa chakula.

Kama alivyosema Waziri Mkuu kwamba uamuzi huo ni wa muda hadi Oktoba, ni vyema wafanyabiashara wakawa wavumilivu. Kama wahenga wasemavyo subira yavuta heri, ni vyema wakakubaliana na serikali kwamba uamuzi uliochukuliwa una nia njema na manufaa kwa Watanzania.

Sambamba na hilo, ni wakati mwafaka sasa hata kwa wananchi ambao walibahatika kuvuna kiasi kidogo kwa ajili ya chakula, hawana budi kutumia kwa uangalifu ndani ya familia ili kujihadhari na baa la njaa linaloinyemelea nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Asante LATRA kwa uamuzi huu ingawa umechelewa

Na Sabato Kasika

**SASA** ni wazi, abiria wanaotumia usafiri wa umma, hasa mabasi, watapata nafuu kama uamuzi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) wa kuzuia mahuburi, biashara na muziki kwa sauti kubwa utafuatwa.

Kwa muda mrefu imekuwa ni jambo la kawaida kwa baadhi ya madereva daladala hasa kufungulia muziki kwa sauti kubwa bila kujali kuwa usafiri huo ni wa umma siyo binafsi na hivyo kukera abiria.

Wale wanaotumia usafiri wa umma kuanzia daladala hadi mabasi makubwa, hakuna asiyejua adha iliyotajwa na LATRA, ingawa ipo nyingine kwa mabasi makubwa ya mikoani kuzidisha abiria hadi wanakosa pa kukaa.

Kwenye suala la adha zote kwa ujumla, nitazungumzia zaidi zilizomo ndani ya daladala, hasa za jijini Dar es Salaam, kuanzia kufungulia sauti kubwa ya muziki, baadhi ya madereva na makondakta kuvutaa sigara na lugha chafu.

Limekuwa jambo la kawaida kwa baadhi yao kufungulia muziki kwa sauti kubwa na hata wakiombwa wapunguze wanagomba au kumwambia abiria anayelalamikia sauti kubwa ashuke atafute usafiri mwingine.

Pamoja na hilo, wapo madereva ambao wanavuta sigara wakiwa wametoa vichwa nje ya dirisha na kupuliza moshi nje ambao husambaa na kwenda kwa abiria waliomo katika daladala, hali ambayo inahatarisha afya zao.

Baadhi ya makondakta nao wakati mwingine husimama nje ya mlango wakiita abiria huku wanavuta sigara, bila kujali kuwa moshi wanaoutoa unasambaa hadi kwa abiria wao. Hivyo hilo nalo lingefuatiliwa.

Ninaamini kwamba usafiri wa umma ukiwamo wa daladala na mabasi makubwa, unalenga kuwasaidia kusafirisha abiria kwenda katika shughuli za kila siku kwa usalama na amani.

Lakini unapojitokeza mtindo wa kufungulia muziki kwa sauti ya juu na mambo mengine ambayo hayatakiwi kufanywa ndani ya vyombo vya usafiri wa umma kama hivyo, ni vyema wahusika wakatambua kuwa hiyo ni kero.

LATRA inaweka wazi kuwa iwe ni mahubiri ndani ya mabasi na mengine ambayo ni kero kwa abiria, hayahitajiki, na kwamba endapo ikibainika kuwa basi linafanya huduma hiyo, hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa dereva na mmiliki wa gari husika.

Lakini pamoja na hayo, ninadhani kuna sababu inayochangia kuwapo kwa hali hiyo ikiwamo baadhi ya madereva na makondakta, kutojua kuwa ni kosa kisheria kuruhusu kelele hizo au kuvuta sigara ndani ya usafiri wa umma.

Hivyo, si vibaya mamlaka husika ikawa na utaratibu wa kuwaelimisha, elimu hiyo pia ifike kwa abiria, hasa wale ambao wamekuwa wakishabikia vitendo hivyo vikiwamo vya mwendokasi katika mabasi makubwa na daladala.

Imekuwa ikidaiwa kuwa baadhi ya abiria hushabikia mwendokasi ili wawahi kufika kule wanakokwenda bila kujali kwamba hali hiyo inaweza kusababisha ajali. Hivyo hao nao wangeelimishwa waachane na mtindo huo.

Wakielimishwa wakaelewa na kuzingatia elimu hiyo, wanaweza kusaidia kupunguza kero ndani ya usafiri huo, kwa kutoa taarifa kwa mamlaka husika wanapoona madereva wanakwenda kinyume.

Ikumbukwe kuwa kwa upande wa kelele za muziki katika usafiri wa umma, Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Selemani Jaffo ameshaweka wazi kuwa zina madhara kwa abiria.

Katika ufafanuzi wake, anasema kelele na mitetemo isiyo ya lazima kwenye mabasi husababisha abiria kukosa utulivu, kutokulala, kuongezeka kwa mapigo ya moyo na kuchangia uwapo wa shinikizo la damu. Waziri anasema ni muhimu kuzingatia kanuni zilizowekwa ili kulinda afya za binadamu kuwaepusha na madhara ya afya ya akili na msongo wa mawazo, na pia anahimiza utunzaji wa mazingira kwa ujumla.

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Kumpongeza Rais kwa mambo mazuri si kunyemelea uteuzi



Na Pascal Mayalla

SERIKALI zote duniani zinaundwa na mihimili rasmi mitatu ambayo ni serikali, bunge na mahakama lakini kuna mhimili wa nne usio rasmi unajulikana kama 'The Fourth Protocol' au "The Fourth Estate'.

Ile mihimili mitatu ni rasmi kwa sababu ndiyo iliyomo kwenye katiba na wakuu wa mihimili hiyo wanatambulika rasmi na kuheshimika sana. Hawa ni Rais, Spika na Jaji Mkuu. Ule mhimili wa nne kwa vile si rasmi, si tu hautambuliki, bali hauna hata mkuu wake lakini upo.

Mihimili hii mitatu ambayo ni rasmi, inaheshimika na majukumu yake, nguvu zake, mamlaka yake na madaraka yake yako wazi kwa sababu yameainishwa kwenye katiba. Lakini mhimili kwa vile hautambuliki, nguvu yake, madaraka yake na mamlaka yake hayatambuliki lakini kiukweli yapo na una nguvu fulani kubwa kuliko hata hii mihimili mingine yote ila nguvu hii haijulikani rasmi kwa sababu ya kutokuwa rasmi.

Mhimili huu wa nne usio rasmi ni vyombo vya habari. Mhimili huu japo haujatajwa rasmi ndani ya katiba yetu, kazi yake imetajwa ndani ya Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) ya mwaka 1977 chini ya ibara za haki za binaadamu kuwa kila mtu ana haki ya kupata habari.

Mhimili huu wa nne, ndio kiunganishi kikuu cha mihimili rasmi mitatu ya dola na wananchi. Kuna kitu kikubwa muhimu kuhusu taifa lolote ambacho siku zote kinasahaulika, wengi wakidhani kitu muhimu zaidi kwenye taifa lolote ni taifa lenyewe tu yaani eneo!

Mfano wa makala hizi za 'Kwa Maslahi ya Taifa'. Tunapozungumzia maslahi ya taifa unamaanisha maslahi ya taifa la Tanzania, hivyo Tanzania ndio inahesabika kuwa ndiyo kila kitu. Lakini kiukweli kabisa, kitu ambacho ndicho kila kitu hata kabla ya taifa lenyewe ni watu, kwa maana ya Watanzania. Watu hawa, Watanzania, ndio wamiliki wa nchi ya Tanzania na ndio wenye ardhi yote ya Tanzania, yaani hii nchi ni mali yao.

Hawa wananchi wa Tanzania, ndio wenye Katiba. Ukiisoma Katiba ya JMT, neno la kwanza kwenye Katiba ni "We The People" (Katiba iliandikwa kwanza kwa Kiingereza ndipo ikatafsiriwa kwa lugha ya Kiwahili), hivyo kitu muhimu cha kwanza ni watu. Watu ndio wenye nchi, ndio wenye katiba, hivyo ndio wenye hii mihimili yote mitatu rasmi na huu mhimili wa nne usio rasmi.

Mhimili huu wa nne usio rasmi, ndio mhimili kiunganishi kati ya mihimili hiyo mitatu rasmi ya dola na wananchi. Nasema hivyo kwa sababu ni sisi waandishi wa habari ndio tunawapelekea taarifa za kutoka mihimili yote mitatu na kuwafikia wananchi. Hata kukitokea jambo lolote kutoka kwa wananchi kwenda kwa serikali yao, ni sisi tena waandishi wa habari tunawafikishia serikali mrejesho kutoka kwa wananchi. Kwa mantiki hiyo, mhimili huu wa nne ndio muhimu kuliko hata hiyo mihimili rasmi.

Kazi rasmi za vyombo vya habari za kiasili ni kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha lakini kazi za kisasa za mhimili huu ni kuibua mambo na kufanya kazi ya ulinzi na kupaza sauti juu ya masuala mbalimbali yaliyomo katika jamii hasa kutoka katika mihimili rasmi mitatu. Kwa maneno ya Kiingereza ni 'the watchdog', yaani mbwa wa hii mihimili mitatu ikikosea, mhimili wa nne ndio wenye uwezo wa kukosoa na kuisaidia jamii.

Hata hiyo mihimili mingine rasmi inapotaka mambo yao yafahamike katika jamii, inautumia sana huu mhimili usio rasmi kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Jiulize ni nani asiyeita waandishi wa habari kama ana jambo lake awe mwanasiasa, msomi, taasisi za kibiashara na kifedha? Hata wananchi wa kawaida wanapobaini hawatendewi inavyotakiwa wanakimbilia kwenye mhimili wa nne kupaza sauti zao. Hapo ndipo unapoona umuhimu wa mhimili huu.

Nchini Marekani, mathalan, mhimili wa nne unaheshimiwa sana na umejijengea heshima kubwa. Ni mhimili uliowahi kumshikia bango Rais wa nchi hiyo, Gerald Ford, aliyefanya makosa fulani kwenye uchaguzi wa Marekani na gazeti la The Washington Post likaripoti kashfa iliyoitwa 'Watergate'. Habari hiyo ilimfanya rais huyo afungashe virago vyake na kuikimbia Ikulu ya Marekani. Kwa maana hiyo, chombo cha habari ndicho kilichosababisha akakaa pembeni.

Hata Tanzania vyombo vya habari vinafanya kubwa nzuri ya kuhabarisha, kuelimisha, kuburudisha, kukosoa na kushauri kupitia tahariri, maoni ya wahariri, habari za uchunguzi na makala mbalimbali elimishi zinazoandikwa na waandishi nguli, mimi nikiwamo.

Rais wetu Samia Suluhu Hassan ameonyesha kwa kauli na vitendo kuwa yeye ni mtu msikivu na kuna mazuri mengi ameyafanya na anaendelea kuyafanya, yanayostahili pongezi. Vyombo vya habari hivi vimemtendea haki kwa kueleza mazuri anayofanya, mara nyingi vikibainisha kuwa 'Mama anaupiga mwingi'.

Kumpongeza huko kwa mazuri anayofanya, yamegeuka shubiri kwa baadhi ya wanahabari na vyombo vya habari kwa ujumla. Tunanyooshewa vidole kuwa tunanyemelea uteuzi wa ukuu wa wilaya, ukuu wa mkoa, ukurugenzi wa halmashauri au ukatibu tawala wa mkoa au wilaya!

Kwa vile mimi ni Mtanzania na nina sifa za kustahili kuteuliwa nafasi yoyote ya uteuzi, kwa sababu ni haki yangu, binafsi naweka wazi kwamba mimi Pascal Mayalla, sipongezi kwa kutafuta uteuzi wowote wa Mama.

Kwa vile kwa sasa niko Mbeya kwenye maonyesho ya Nanenane na Mama Samia pia yuko Mbeya na ndiye atakayefunga maonyesho haya, ikitokea nikakutana naye, kwanza nitamsalimia 'Shikamoo Mama. Pili, nitampongeza kwa kazi nzuri na tatu nitamwambia wazi kabisa Mimi Pascal Mayalla sitaki uteuzi wowote.

**Wasalaam.**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Watanzania kwa nini kudanganyana huku?



Na Joseph Kulangwa

**Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, enzi zake alipata kuja na usemi wa Kizanaki kuwa: "Ombhisabhisa obhurweri ekriro kiimbura." Akimaanisha kuwa mficha maradhi kilio humuumbua.**

UONGO au kudanganya ni tabia mbaya sana kwa binadamu. Ni tabia ambayo inamfanya mtu aishi maisha bandia, akitaka kuonekana anacho kumbe hana.

Wapo watu ambao unaweza kuwaona wana mali kumbe za kuazima nia ni kutaka kuonesha jamii kwamba wana maisha wanayoita ya matawi, lakini kumbe si chochote si lolote.

Hao ni wale ambao siku ya siku ikifika wakagundulika, hubaki kuziba nyuso zao kwa viganja kama kina Adili na nduguze, walioficha nyuso zao kwa aibu.

Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, enzi zake alipata kuja na usemi wa Kizanaki kuwa: "Ombhisabhisa obhurweri ekriro kiimbura." Akimaanisha kuwa mficha maradhi kilio humuumbua.

Alikuwa akimaanisha mtu kuwa na uhalisia wa maisha, badala ya kujipamba makubwa yaliyo nje ya uwezo wako, na matokeo yake ni kuumbuka na kujikuta na aibu na kupata shida.

Fikiria mtu ana kaswende lakini kwa kuona aibu hataki kusema ili apate tiba, badala yake anavumilia huku ugonjwa ukimtafuna na utafika wakati anashindwa kuvumilia, akifunguka tayari amechelewa na ameathirika kwa kiwango kikubwa.

Sawa na mtu mzima asiyejua kusoma lakini hataki kujifunza kusoma. Kwa kuona aibu kuwa na utu uzima alionao ni aibu kuchanganyika na watoto kusoma na matokeo yake, anabaki na ujinga wake na siku akiwa peke yake akapelekewa barua kusoma, ndipo anapoadhirika na anaweza hata kusomewa na kudanganywa.

Hii ni tabia iliyoota mizizi si tu kwa mtu mmoja mmoja lakini inashangaza kumbe inaweza kuwa hata katika jamii mpaka ngazi ya kitaifa, hivyo kusababisha mshangao kwa wanajamii husika.

Kwa mliomsikia Chifu Hangaya hivi karibuni wakati akiapisha wasaidizi wake wa mikoani aliowateua katika mabadiliko aliyofanya, katika hotuba yake akagusia mashirika ya umma yalivyofanya enzi za mtangulizi wake.

Mama bila kumung'unya maneno, akayanyooshea kidole mashirika ya umma yaliyojifanya yanatoa gawio enzi za JPM kumbe magumashi. Akasema baadhi yalilazimika kwenda benki kukopa ili kuwasilisha gawio serikalini.

Eti kwa kuchelea kumwaga unga au kuweka mchanga kwenye kitumbua, watendaji wa mashirika na taasisi za umma, walibisha hodi kwenye benki kukopa, ili kuonekana wako imara kiuchumi kumbe hakuna kitu ili mradi kumridhisha JPM!

Unajua kabisa shirika unaloongoza hakuna kitu, haliingizi faida bali hasara tupu, katika donda hilo unaongeza chumvi kwa kwenda kuongeza mzigo wa deni benki, hivi wakati unalipa deni huko watumishi wako unawalipa nini?

Watanzania tunaweza sasa kujiuliza kulikuwa na haja gani kutupaka mafuta kwa mgongo wa chupa? Yaani tulifanywa mazwazwa kuoneshwa kuwa mashirika yanaupiga mwingi mpaka kutoa gawio kumbe changa la macho!

Tunaweza kujiuliza kama ni hivi tulidanganywa mangapi enzi hizo ambazo watu walifanya kazi kwa nidhamu ya uoga mpaka kufikia kujibebesha magunia ya misumari kama hivi? Yaani mtu unachomwa misumari ya kichwa lakini husemi unagugumia mpaka mzigo ufike!

Chifu Hangaya ni kiongozi wa aina yake, asiyetaka kudanganya watu wake, kama ilivyotokea kabla yake, ambapo sasa ameamua kuwaambia kwa uwazi viongozi wa mashirika hayo, kuchapa kazi na si kukalia kudanganya tunazalisha kumbe ufisadi mtupu.

Kwa hiyo Watanznaia tulidhani mashirika yanafanya vizuri katika kujenga uchumi wetu, kumbe hakuna kitu na ndiyo sababu watu walikuwa wanalia mambo magumu, mifuko haina ndururu, kumbe ni kutokana na uongo huu!

Tukanunua midege kwa mwendokasi, lakini kumbe yote ilikuwa ni kutufumba macho tuko vizuri, lakini hatukujua tunaficha maradhi na kama tungeendelea hivyo, basi kilio kingetuumbua tu kwa vyovyote na sijui tungelaumiana au tungemlaumu nani!

Sasa basi ili tusifukue makaburi, ni vema sasa mliopewa majukumu na dhamana ya kututumikia wananchi, tusimwangushe Chifu Hangaya, tupige mzigo bila kujiingizia madeni ya kudanganya kuwa tunazalisha mpaka kutoa gawio, kumbe hakuna kitu.

Kumbe ndiyo sababu JPM akamkalisha chini Msajili wa Hazina na kumwagiza atumie sheria zinazomsimamia, kuhakikisha mashirika yasiyotoa gawio ama yanafutwa au kufilisiwa na watendaji kumwaga unga!

Hata kama ni wewe una familia yako na unajua kiti unachokalia ndicho kinahakikisha mkate wa kila siku uko mezani, halafu uambiwe bila kupeleka gawio utaula wa chuya utafanyaje? Utadanganya tu. Kweli Watanganyika Wadanganyika! Alamsiki!

Na Dk. Enock Mlyuka

# Migogoro ya ndoa kichocheo kikubwa magonjwa ya akili

NDOA ni taasisi ambayo Mungu alianzisha ili watu waingie, waipende na kuifurahia kwa sababu ni jambo ambalo makusudi yake ni watu kuishi katika furaha na amani na si jukwaa la masumbwi au uwanja wa vita.

Amani ni msingi wa wema, heshima na maendeleo endelevu. Kwa mantiki hiyo, amani ni zawadi inayopaswa kutunzwa kwa kuwa na ndoa imara na malezi yenye dhamira nyofu kwa kulinda na kuheshimu utu wa binadamu, ustawi na maendeleo ya familia, jamii na taifa kwa ujumla.

Ndiyo maana hata wakati wa mchakato wa uchumba hadi ndoa, amani hutawala na ni nadra kusikia wachumba au wanandoa watarajiwa wanagombana na kupigana. Aidha, katika ndoa. mume na mke ni watu wanaotegemeana. Mungu aliumba mwanamume na mwanamke ili wahitajiane na kutegemeana katika maisha; wafurahi na kufurahishana.

**KUIBUKA MIGOGORO**

Pamoja na kusudi zuri la Mungu la kuanzisha taasisi ya ndoa ili wanandoa waishi kama paradise, wanadamu wameharibu misingi na ladha yake. Hali hii inapotosha kwa kiasi kikubwa kusudi na maana halisi ya taasisi hii takatifu. Kwa baadhi ya familia, ndoa zimegeuka jela ya nyumbani kutokana na migogoro ya mara kwa mara isiyo na ukomo. Migogoro hiyo imekuwa sasa mtindo wa maisha.

Takwimu za Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Watoto na Makundi Maalum zinaonyesha kwamba hadi Aprili, mwaka huu, ilipokea migorogo 39,571 ya ndoa na kati ya hiyo, migogoro 19,262 ilipatiwa suluhu, 15,718 bado iko katika usuluhishi, huku 4576 ikiwa mahakamani. Hii ni dhahiri kwamba migogoro ya ndoa inaongezeka na hata kuwa janga la kitaifa.

Kimsingi, migogoro ya ndoa hujeruhi nafsi, huondoa hisia za mapenzi na mvuto miongoni mwa wanandoa. Hali hii huchangia matatizo ya afya ya akili kwa sababu ya msongo mkubwa wa mawazo. Magonjwa ya akili ni kichocheo cha watu kufanya vitendo vya ukatili na mauaji miongoni mwa wanandoa.

Matukio ya ukatili yanapotokea, katika jamii hayaathiri wanandoa pekee, bali na watoto waliozaliwa katika ndoa hizo kwani mfumo wao wa maisha unavurugwa. Halikadhalika, wazazi na familia wanazotoka wanandoa huathirika pia kwani hakuna mzazi ambaye angependa kuona mtoto wake anapata matatizo.

Magonjwa ya akili yanaweza kusababishwa na mambo ya kibailojia au kisaikolojia kama vile kurithi vinasaba kutoka kwa wazazi, magonjwa ya muda mrefu, matumizi ya dawa za kulevya, uvutaji bangi na ulevi wa pombe kwa sababu madhara yake huenda moja kwa moja kwenye ubongo; na migogoro ya mara kwa mara isiyokoma.

Sababu zingine ni pamoja na vitendo vya ubakaji, unyanyasaji, ukatili wa nyumbani (domestic violence), msongo wa mawazo wa muda mrefu, ugumu wa maisha kama vile majanga, kukosa au kupoteza ajira.

Kwa upande wa watoto, unyanyasaji wa kingono, kukosa matunzo stahiki, ugomvi wa mara kwa mara wa wazazi wao, kutokuthaminiwa na kutelekezwa huwaathiri sana watoto kisaikolojia na kusababisha matatizo ya afya ya akili wangali wadogo. Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonesha kwamba, takribani asilimia 20 ya watoto na vijana duniani wana matatizo ya afya ya akili.

**HALI ILIVYO**

Kwa mujibu wa Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) za hadi mwaka 2022, takribani watu bilioni moja wanaishi wakiwa na magonjwa ya akili (mental disorders). Kati ya watu wanne, mmoja ana tatizo la afya ya akili.

Taarifa ya Mpango wa Taifa wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza zinabainisha kuwa idadi ya wagonjwa wa akili imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Mwaka 2018, kwa mfano, kulikuwa na wagonjwa 357,799 na mwaka uliofuata waliongezeka hadi kufikia 380,000 na mwaka 2020 walifika zaidi ya 500,000.

Hizi ni takwimu za wagonjwa waliofika hospitalini kupatiwa matibabu. Inawezekana wenye matatizo haya ni wengi katika jamii kwa sababu ya uelewa mdogo wa watu wengi kuhusu magonjwa ya akili.

**DALILI**

Dalili za magonjwa ya akili ni pamoja na wivu uliopitiliza, kuhisi maisha kutokuwa na thamani na mtu kutamani kufa au kuua kuliko kuishi; kuwa na woga na wasiwasi kupita kiasi; kuongea au kutokuongea kupita kiasi; hasira kali za haraka; mtu kujitenga na wenzake na kupenda kukaa mwenyewe muda mwingi; kutokujijali kwa usafi na muonekano wa nje; kukosa usingizi au kulala usingizi sana kupita kiasi; kusahausahau vitu na kupoteza kumbukumbu; kuwa na imani zisizo za kawaida, na mawazo kukosa mtiririko unaoeleweka.



Mungu alianzisha ndoa ili watu waishi kwa amani, upendo na furaha.

**NINI KIFANYIKE?**
**ELIMU NA UPIMAJI AFYA**

Migogoro ya ndoa inahitaji kupatiwa ufumbuzi mapema ili kuwaepusha wanandoa na athari zitokanazo na migogoro. Ni muhimu watu wajenge utamaduni wa kupima afya ya akili kabla ya ndoa kwa sababu wako baadhi ya watu wamezaliwa wakiwa na matatizo ya afya ya akili. Kuongezeka kwa vitendo vya ukatili na mauaji ya wanandoa katika familia ni kiashiria kuwa, baadhi ya watu wameoa au kuolewa na watu wenye matatizo ya afya ya akili.

Elimu kwa umma kuhusu masuala ya afya ya akili inabidi kutolewa ili kuwasaidia wananchi kujitambua kwani watu wengi bado hawana ufahamu wa kutosha kuhusu tatizo hili. Matokeo yake watu hawaoni umuhimu wa kupima na kujua hali zao za afya.

Taasisi ya ndoa ni taasisi nyeti yenye misingi, kanuni, sera, taratibu na miiko yake. Ni muhimu watu watamani na kudhamiria kujifunza kwa lengo la kuifahamu vizuri taasisi hii kabla ya ndoa ili kuepuka matatizo yasiyo ya lazima.

Watu wengi wameoa au kuolewa pasipo kuwa na ufahamu na maarifa ya kutosha kuhusu taasisi ya ndoa matokeo yake wamekuwa vivuruge. Nguvu kubwa huelekezwa katika kuandaa sherehe za harusi na siyo kujiandaa kuwa mume na mke bora.

**UHUSIANO NA MUNGU**

Suala la usalama katika ndoa ni jambo muhimu, wanandoa wafahamu kwamba, hakuna usalama katika ndoa Mungu asipohusika. Hivyo, wanandoa wawe na uhusiano mzuri na Mungu na wao kwa wao ili wawe salama. Kutokuwa na uhusiano mzuri na Mungu kunawaondolea wanandoa kinga ya kiroho na hofu ya Mungu ndani yao. Kinachobaki kati yao ni kuumizana na kukosa roho ya msamaha.

**MSAMAHA NA KUSAMEHE**

Ndoa ni safari ya maisha ambapo kuna kukosea na kukosana njiani. Ni muhimu wanandoa wawe wepesi kujifunza, kujikosoa, kujisahihisha na kuombana msamaha pale mtu anapohisi kumkosea mwenzake.

Msamaha ni dawa ya furaha ya familia. Msamaha ni muhimu kwa afya yetu ya kihisia na kuendelea kuishi kwa heri. Asiyeomba msamaha na asiyesamehe hana amani katika nafsi yake na hawezi kuwa na ushirika na Mungu. Pia, mtu wa aina hiyo hawezi kuwa na uhusiano mwema na binadamu mwenzake.

Watu wasioomba msamaha na wasiosamehe ni wagonjwa wa kimwili, kihisia na kiroho. Siku zote huteseka na kuishi kwa vinyongo na roho ya visasi na maangamizi. Bila msamaha, familia inakuwa uwanja wa migogoro, ngome ya uovu na maafa.

Migogoro ya ndoa ni adui wa maendeleo kwani maendeleo na ustawi wa familia na taifa unategemea ndoa imara. Kwa hiyo, ni muhimu kila mwanandoa ajiheshimu, atambue nafasi, wajibu na mipaka yake katika ndoa ili kuifanya ndoa kuwa baraka.

**■Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**



Migogoro mingi ya ndoa imekuwa chanzo kikubwa cha magonjwa ya akili.

# MAISHA

AGOSTI 7, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 13

**Fulana, Denim ya Jeans ni hatari**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Bomba za pazia zinavyonogesha



Ukurasa 12

**HARUSI**




## RUDISHA NGOZI ASILI


# Tango, nyanya, asali vitakupa furaha

Ukurasa 14

## WATOTO

### MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | D | I | M | B | A |
| | O | | | A | |
| O | N | A | | M | |
| | Y | | I | B | A |
| | O | | | I | |
| Y | A | N | G | A | |

### AMSHA AKILI


Tafuta njia ukianzia alama A kuelekea B




### TOA TOFAUTI 5





### FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi: PAO, AKA, PIMBI, SHAKA, KIBALI, SUKARI

## PAKA RANGI




Alichokifanya daktari

MTOTO Juma alikuwa akizungumza na rafiki yake wakitoka shuleni.

**Juma:** Hivi leo umemuelewa mwalimu wa bailojia?

**John:** Nimemuelewa sana tu

**Juma:** Hivi itakuaje wale vikambale vidogo vikageuka kuwa vyura?

**John:** Kaeleza kuwa wale sio kambale bali ni hatua ya ukuaji wa chura, wanaanza kama yai, wanakuja kuwa viluilui na kisha anakuwa chura kamili. Wale sio kambale

**SWALI**

Konokono analeta athari zipi kwa binadamu?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Aliyepora mume wa rafiki yake azaa boga!

***KARIBU tena msomaji wangu tuzidi kumulika jinsi maisha yalivyo kwenye familia zetu. Mwishoni mwa safu hii, nimekuwa nakaribisha maoni au visa vya kimaisha ili kujifunza mambo mbalimbali kutokana navyo.***

Kijana mmoja aitwaye Selestine, msomaji mzuri wa gazeti hili na pia safu hii, alinisimulia kisa kimoja cha kusisimua kuhusu shangazi yake aliyejifungua boga badala ya mtoto miaka kadhaa iliyopita. Akasema hivi Shangazi yake aitwaye Chrisanta alijifungua boga hospitalini jambo ambalo lilishangaza wengi. Na kisa cha mkasa huo ni kwamba alipora mume wa rafiki yake. MwanaMume huyo aliitwa Eliezeri Msafiri.

Baada ya rafiki yake huyo kugundua kuwa yule aliyekuwa karibu naye wakicheka na kushirikishana mambo mengi ana uhusiano na mumewe na anammiliki jumla, akatamka maneno yafuatayo: "Ikiwa wewe rafiki yangu umenitendea hivi, sitamwamini tena mtu yoyote, na utaona yatakayokupata."

Shangazi akaendelea kuishi na mwanamume huyo akapata ujauzito. Alipokwenda hospitali kujifungua, badala ya kuzaa mtoto akazaa boga! Baada ya tukio hilo,

> **Waliokwenda kwa shughuli hiyo walikuwa mama yake shangazi, bibi wa Selestine, Eliezeri mume wa shangazi na shangazi mwenyewe aliyezaa boga hilo.**

babu wa kijana huyu akawaita wajukuu zake kuwapa taarifa hizo, kisha akawauliza, je, mnasemaje kiumbe hicho cha ajabu kiletwe nyumbani au kitupwe huko huko? Wakajibu, kiletwe tukione!

Wakati hayo yanaendelea, mume wa shangazi alishaongea na mfanyabiashara wa madini wa Mwadui, Shinyanga kuhusu hilo boga na kukubaliana atampa Sh. 500,000 kisha yeye atalipeleka mgodini. Hata hivyo, mama mzazi wa Eliezeri akashauri atafutwe mganga kufumbua hicho kitendawili, akapatikana mganga kutoka Burundi aliyetafutwa na Eliezeri.

Alipofika mganga huyo akatoa masharti yafuatayo; yatafutwe maziwa freshi lita 60 na ulezi usiopungua kilo tano kwa ajili ya kuchanganywa pamoja ili familia yote iogeshwe. Wakati huo, wazazi wa Selestine walikuwa wanaishi Tanga walikotafuta makazi mapya kwa kukimbia mauzauza ya kijijini.

Mchanganyiko huo kila aliyekuwapo aliogeshwa kuanzia kichwani hadi miguuni. Baada ya hapo mganga akasema litafutwe kaburi la mtoto mchanga kuanzia miezi sifuri hadi sita, lifukuliwe kisha kuchukuliwa sanda yake kwa ajili ya kwenda kulivisha lile boga! Baada ya sanda kuletwa ikaagizwa ifuliwe kwanza kisha shangazi na mumewe wapewe maji yaliyofulia hiyo sanda kila mmoja anywe nusu lita na maji mengine wayaoge usiku, jambo ambalo lilifanyika!

Ndipo ile sanda ikavishwa lile boga tayari kwenda kulizika kule kwenye makaburi ilikochukuliwa ile sanda. Waliokwenda kwa shughuli hiyo walikuwa mama yake shangazi, bibi wa Selestine, Eliezeri mume wa shangazi na shangazi mwenyewe aliyezaa boga hilo. Wote waliokwenda kuzika waliambiwa wasivae nguo yoyote mwilini. Waliporejea toka kuzika yule mganga akawauliza kama walikutana na kitu chochote njiani wakasema hakuna walichoona.

Akatoa masharti tena kwamba achinjwe ng'ombe jike tasa ili kipikwe chakula watu wale. Alipoletwa na kuchinjwa, akachukua damu ya ng'ombe akawapaka wote kwenye paji la uso na kuwatamkia kwamba mikosi na nuksi vyote vimekwisha!

Mpenzi msomaji wangu, kisa hiki kina mafunzo mengi kwa maisha yetu tunayoishi leo. Labda nitaje maeneo kadhaa ya msingi niliyokaza macho. Awali ya yote, Mwenyezi Mungu katika moja ya maandiko yake anasema watu wangu wanaangamia kwa sababu ya kukosa maarifa. Bado watu wengi wako gizani fahamu zao zimefungwa kutambua madhara ya kile wakifanyacho.

Mungu ameweka amri zake akasisitiza kuwa tusiabudu miungu mingine ila yeye. Lakini bado watu wanaendekeza ushirikina wakiamini kuwa ndiyo njia sahihi kuwafanikisha kimaisha.

Familia ya shangazi hawakuwa washirikina lakini walijikuta wanaangukia kwenye boma linaloamini mambo ya uganga kuwa kinga yao. Angalia mume aliyempora ndiye aliyetaka kuuza lile boga, ndiye aliyetafuta mganga. Mungu anasema kwenye moja ya maneno yake, na alaaniwe anayemtumainia mwanadamu kuwa kinga yake. Pia akasema mwanamke mchawi asiishi. Wote waliokwenda makaburini kwa kisa hiki walishatangulia mbele za haki.

Jambo lingine la kujifunza ni kuhusu nguvu ya maneno. Maneno aliyotamkiwa shangazi ndiyo yaliyoharibu hatma ya maisha yake. Maneno aliyotamkiwa na rafiki yake kwamba "utaona kitakachokupata' yalikuwa ni mwiba mkali uliozima ndoto ya shangazi yule. Tumtafute sana Mungu ambaye anaweza yote.

***Msomaji wangu, tuishie hapa. Wiki ijayo nitakuletea kisa kingine cha kijana huyu huyu kuhusu maisha yake. Je, una maoni, kisa? Ujumbe mfupi 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Nanenane iwe chachu kuboresha kilimo

KESHO ni maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima, maarufu kama Nanenane ambayo hukusanya wadau kutoka maeneo mbalimbali kwenda kuonyesha kazi zao ambazo zinasaidia kuchechemua kilimo.

Licha ya kuwa na maadhimisho kitaifa yanafanyika jijini Mbeya, kila kanda maadhimisho yanaendelea kwa taasisi, mashirika, watu binafsi na wakulima mmoja mmoja kuonyesha kazi zao ambazo ni muhimu kwa taifa.

Unapotembelea maonyesho hayo utaona kazi nzuri za shambani ambazo unatamani mavuno yangekuwa hivyo siku zote.

Kama haitoshi kuna mashamba darasa ambayo kila halmashauri ina shamba lake imependa zao la mfano ambalo ni kwa ajili ya kuwafundisha watu wanaotembelea maonyesho hayo.

Aidha, watafiti hubainisha utafiti waliofanya na kwa namna gani zinaweza kuleta matokeo chanya ikiwa zitafika kwa wakulima na hivyo kuboresha au kuongeza uzalishaji.

Pia wabunifu mbalimbali huonyesha kazi walizozifanya ambazo zina nafasi kubwa ya kuleta mabadiliko kwenye jamii, kutoa suluhisho la mambo mbalimbali kwa kutumia gharama ndogo kuliko kuagiza teknolojia kutoka nje.

Kwa ujumla, maadhimisho ya Nanenane ni muhimu sana kwa maendeleo yetu, ikiwa yatatumiwa vyema itasaidia sana elimu kuwafikia wengi kwa urahisi.

Mathalani, Aprili, mwaka huu, serikali iligawa pikipiki kwa maofisa ugani nchi nzima, lengo ni kuhakikisha wanawafikia wakulima kwa haraka na kutoa elimu sahihi ya ugani ambayo itaboresha kazi zao.

Pia, kwenye bajeti ya Wizara ya Kilimo, vimewekwa vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2022/23 kwa ajili ya kuleta mapinduzi kwenye kilimo, kuimarisha utafiti na ubunifu utakaotoa suluhisho kwenye matatizo ya jamii.

Naamini vipaumbele hivyo vikitekelezwa kwa dhati nchi itapiga hatua kubwa kwenye uzalishaji wa chakula na kuyafikia masoko kwa urahisi zaidi, hali itakayoboresha maisha ya mtu mmoja na taifa kwa ujumla.

Nawaza kwa kiasi gani mashamba ya kwenye maonyesho yanasaidia kubadili kilimo. Mara nyingi utaona mashamba ya halmashauri yana mazao mazuri sana lakini ukitembelea maeneo yao halisi hawana hayo mazao na uzalishaji ni wa chini.

Unapotembelea maonyesho hayo utaona mazao mazuri sana kiasi kwamba unapokwenda kwenye mashamba ya wakulima huyakuti huwa najiuliza yanaandaliwa kwa ajili ya maonyesho tu au ni uzalishaji endelevu.?

Natambua gharama kubwa sana hutumika kuandaa maonyesho hayo kuanzia watumishi wanaosafiri kulipwa posho, mafuta ya magari, nauli na gharama zingine za uendeshaji.

Ni muhimu ubora wa mazao unaoonekana ukawafikia wakulima kwamba mbinu za kuboresha mazao katika eneo dogo zikaelekezwa kwenye mashamba ya wakulima, naomba 'waambukizane' elimu hiyo muhimu ambayo itawawezesha kuboresha kilimo.

> **Kwa ujumla, maadhimisho ya Nanenane ni muhimu sana kwa maendeleo yetu, ikiwa yatatumiwa vyema itasaidia sana elimu kuwafikia wengi kwa urahisi.**

Tuko katika wakati wa mabadiliko ya tabia nchi, mvua hazitabiriki na wakati mwingine hazinyeshi kabisa, kiasi cha maji kimepungua hali ambayo ni ngumu kwa wazalishaji wote yaani wanaotegemea mvua na umwagiliaji.

Lazima wakulima waelimishwe mara kwa mara ili kujua namna ya kuishi na mabadiliko ya tabia nchi, ambayo hayatarajiwi kuisha leo wala kesho ni suala la dunia ambalo litapunguza uzalishaji wa chakula kwa kiasi kikubwa.

Bila hivyo wengi wataendelea na kilimo cha mazoea ambacho hawatazalisha na kukata tamaa, lazima kuboresha uzalishaji ili watu wawe na uhakika wa chakula wakati wote.

Kilimo ni uti wa mgongo kinapaswa kuendelezwa ili zaidi ya asilimia 70 wanapotegemea shughuli hiyo wazalishe kwa tija na kibiashara, kwa kuwa mahitaji ya chakula ni ya kila siku.

***Mungu ibariki Tanzania***

# HARUSI







Ilikuwa siku ya furaha kwa wazazi, ndugu na marafiki wa Msonge Msilanga, wakati wa sherehe ya kumuaga iliyofanyika Julai 27, mwaka huu katika ukumbi wa Prime Rose, Mbezi jijini Dar es Salaam, na kisha kufunga ndoa na mume wake Yusuf Kaoneka.







## MITINDO



# Fulana, Denim ya Jeans ni hatari



NI aina ya mpangilio mpya wa mavazi kwa wanawake ambao wanataka kuonyesha ujana wao.

Mtindo huu wa mavazi umezidi kusambaa kwa kasi duniani kote, na hata hapa nchini mambo yanazidi kunoga kutokana na idadi kubwa ya vijana wa kike wakitupia.

Hata hivyo, vazi hili huwezi kwenda nalo katika maeneo yenye mikusanyiko ya watu wengi, bali ni maalumu nyakati za jioni au kwenye maeneo ya mapumziko.

Hapa tunazungumzia vazi la Denim ya Jeans na fulana nyepesi yenye umbo la V eneo la shingoni.

Nguo hizi zinabaki kuwa ni nzuri zaidi kuvaliwa na wanawake pekee.

Kimsingi Denim ya Jeans na fulana ya aina hiyo inakupa muonekano wa ujana zaidi na wale wenye umri wa kati wanaotaka kuvaa, ni lazima wajitathmini au kupata ushauri kwa wataalamu wa mavazi.

Mwanamke anapovaa mavazi haya, huwa na muonekano wenye urembo halisi.

Uzuri wa mpangilio huu wa mavazi unamfanya mvaaji kuonekana kuwa na shingo ndefu kutokana na eneo la mabegani kuwa wazi.

UREMBO



RUDISHA NGOZI ASILI

# Tango, nyanya, asali vitakupa furaha

KATIKA shughuli za kila siku suala la miili yetu kupatwa na mionzi ya jua limekuwa jambo la kawaida.

Mionzi hii sio tu huifikia ngozi zetu, lakini pia huweza kusababisha mabadiliko fulani katika ngozi na kuonekana imefifia au kuwa nyeusi zaidi.

Mfano mzuri mtu akitembea juani kwa muda mrefu utaona rangi ya paji la uso liko tofauti na sehemu nyingine au kwa wale wenzetu wanaovaa nguo zinazoacha wazi maeneo ya kifua au mgongo utagundua rangi ya maeneo hayo iko tofauti na sehemu zingine za mwili.

Hali hii inajulikana kitaalamu kama suntanning. Hii hutokea pale ngozi inapozalisha zaidi chembe hai zinazofanya kuwa na rangi nyeusi (melanin), ikijaribu kujilinda dhidi ya uharibifu unaoweza kusababishwa na mionzi ya jua.

Hata hivyo, Leo nimekuandalia njia za asili na rahisi ambazo unaweza kuzitumia ili kusaidia kuondoa utofauti wa rangi ya ngozi unaoletwa na mionzi ya jua.

**Nyanya na asali**

Nyanya kubwa moja na asali (kijiko kikubwa).

Kuna njia mbili unazoweza kutumia kuandaa mchanganyiko huu. Kwanza chukua nyanya, ikate katikati na uchovye asali upande huo ulioukata kisha anza kupaka sehemu husika.

Pili unaweza kuchukua nyanya na kisha uisage, changanya asali na uanze kupaka.

Ukimaliza kujipaka subiri kwa dakika 15 hadi 20 baada ya hapo nawa maji halafu jikaushe kwa kitambaa safi.


Fanya hivyo kila siku kupata matokeo yanayo ridhisha.

**Tango na Asali**

Chukua tango moja na asali kijiko kimoja cha chai. Saga tango kisha changanya na asali.

Paka mchanganyiko huo sehemu iliyoathiriwa, subiri kwa dakika 10 hadi 15 kisha nawa maji.

Tumia njia hii mara moja au mbili kila siku.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Utamu wa makaroni

MAKARONI ni chakula rahisi kuandaa na hakitumii muda mrefu kupika.

Chakula hiki ni kizuri, chenye afya na bora kutumiwa na watu wa rika zote.

**Mahitaji**

Makaroni nusu, pima kutokana na mahitaji yako, nyanya nne zilizoiva vizuri, nyanya za kopo vijiko vitatu, vitunguu maji viwili na kitunguu saumu kimoja

Pilipili hoho moja, soy sauce kijiko kimoja kidogo, chumvi kijiko 1 kidogo, giligilani kijiko kimoja, masala robo kijiko kidogo,Curry powder kijiko kimoja kidogo na tangawizi nusu kijiko kidogo

Nazi moja iliyokomaa, njegere glass moja, bilinganya moja, kate vipande virefu na vyembamba, Italian seasoning kijiko kimoja kidogo, pilipili ndefu mbili, na Cayenne pepper kijiko kmoja kidogo.

**Maelekezo**

Unaweza kuongeza viungo unavyopendelea ili kukifanya chakula kiwe kitamu.

Ila kama unakula na watoto, hakikisha unapunguza uwingi wa pilipili, maana watoto hawatahimili ukali wake.

Andaa viungo, menya nyanya,vitunguu maji 2, pilipili hoho na kitunguu saumu. Kata vipande vidogo, hifadhi pembeni. Kamua tui zito la nazi, hifadhi pembeni.



Andaa njegere, zichemshe. Ila zisiive sana, epua na weka pembeni.

Kwenye sufuria, weka maji na chumvi, acha yachemke. Weka makaroni, pika kwa dakika saba hadi nane (fuata muda elekezi kwenye packet ya macaroni) kisha epua. Chuja maji, hifadhi pembeni.

Ni vizuri ukipika makaroni dakika 1 au 2 chini ya muda elekezi kwenye packet, hii itafanya makaroni yaive vizuri yakichanganywa na sauce na wakati wa kumalizia kupika.

Weka mafuta ya kula kwenye sufuria, bandika jikoni. Acha mafuta yapate moto vizuri kisha weka kitunguu maji.

Hakikisha moto ni mkali ili mboga ziive vizuri bila kuchuja maji.

Pika kwa dakika mbili huku unakoroga. Weka kitunguu saumu, curry powder, tangawizi, pilipili ndefu, giligilani ya unga, Italian season na gharam masala. Koroga vizuri kisha weka nyanya. Koroga vizuri kisha acha ziive hadi zitengane na mafuta. Weka nyanya ya kopo (tomato paste) na bilinganya, koroga pamoja.

Weka njegere, koroga pamoja, soy sauce pamoja na chumvi kiasi na makaroni kwenye sufuria.

Changanya na uji wa yanya na njegere, weka pilipili hoho, koroga na acha ziive kiasi, ili harufu iwe tamu na nzuri.

Weka tui la nazi, geuza mara kwa mara kisha acha chakula kichemke kidogo na nyunyizia cayenne pepper na pilipili manga ichanganye na chakula kisha epua.

Chakula kitakuwa tayari ili upate ladha zaidi, kula chakula hiki kikiwa bado cha moto.

## MAISHA NI NYUMBA
Na Elizabeth Zaya

# Bomba za pazia zinavyonogesha



DUNIA ya sasa inatawaliwa na uzuri na mambo yanayovutia, ndiyo maana hata jinsi unavyofunga pazia unatakiwa kuwa makini ili kuifanya nyumba ipendeze zaidi.

Ni rahisi kutokujali namna pazia na bomba zake zinavyowekwa ili chumba kionekane vizuri au kisivutie. Ila pale utakapoziondoa ndipo unagundua umuhimu wake.

Zifuatazo ni dondoo chache za namna ya kuchagua mabomba ya pazia unazotaka kutundika iwe chumbani au sebuleni.

**1:** Hakikisha unaweka ambazo zinaendana na mapambo mengine yaliyoko sehemu inakofungwa pazia husika. Hapa ni muhimu kuangalia rangi na muundo.

**2:** Usinunue bomba ya rangi ya dhahabu kwa mfano, isioane na chochote hapo chumbani na ikawa kama kitu kisicho mahali pake.

**3:** Jali mwonekano wa mwisho uliotumika kupendezesha bomba hizo. Utagundua kuwa bomba zenye muonekano usio wa kung'aa zinatengeneza mandhari tulivu kuliko ule wa kung'aa wa polishi.

**4:** Huna haja ya kununua fimbo za gharama kubwa, zote kazi yake moja. Cha muhimu ni kuzingatia urahisi wa kufunga na kufungua pazia ikiwa imetundikwa kwenye fimbo hiyo.





# Hivi ndivyo unaweza kutumia vizuri kona chumbani kwako

KILA kona ya chumba iliyo tupu ni fursa yako kubuni namna ya kuipendezesha.

Wakati unaipendezesha una fursa ya kuitumia pia hata kama awali ilikuwa inaonekana haiwezi kufaa kwa matumizi. Ziko njia nyingi za namna ya kubuni kutengeneza kona yako ikapendeza na hata kupendezesha nyumba yako pia.

Njia mojawapo unaweza kuamua ukaitumia kama shelfu ya kuhifazia vitabu vyako kwa kuitengeneza kufuatisha muundo wa kona.

Hii ni moja ya njia nzuri kufanya isiyokuwa na kitu itumike na shelfu zinaweza kutengenezwa kwenda juu karibu na dari kulingana na mahitaji na ukubwa wa kona ya nyumba yako.

Mbali na shelfu za vitabu, pia unaweza kutengeneza kona yako kwa ajili ya kuweka mapambo madogo.

Pia kona inatumika kutengeneza sehemu ya kufanyia shughuli mbalimbali za kiofisi au kusomea.

Kumbuka sehemu ya kona ikitengenezwa vizuri ni nzuri zaidi na hutuliza akili hususani kwa wanaosoma. Pia unaweza ukaitumia kona kama sehemu ya kutundika picha za familia.

Huhitaji ukuta mkubwa kwa ajili ya kusambaza picha za familia yako badala yake tumia kona hiyo kuongeza mvuto na pia usiweke nyingi zikakuharibia mvuto.

Pia unaweza kuweka ua la mmea wa kuoteshwa endapo hutataka kuweka shelfu au sanaa zozote na itasaidia kuingiza uoto asili ndani ya nyumba kwa sababu matawi yake yatatosha kuijaza kona yenyewe.



Kwenye chumba, kona hiyo unaweza kuitengeneza vizuri kama sehemu ya kutundikia nguo hasa kwenye chumba cha kunyooshea au kinachotumika kwa ajili ya kulala.


Hata katika chumba cha wageni ambacho mara nyingi huwa sio kikubwa, unaweza kuitumia kupachika hata mbao nyembamba inayoweza kukutanisha pande zote mbili za kuta na hapo ukatundika nguo zako na zikakaa katika muonekano mzuri.

Na kwa wenye sebule au vyumba vyenye nafasi ndogo, kona inafaa pia kuweka sofa hasa la duara lenye vipande viwili ambavyo vinaunganika.

Pia unaweza kupendezesha kona yako kwa kuweka vinyago ambavyo navyo lazima uweke juu ya meza ndogo au ukapatengenezea kabati au meza ya miguu mitatu.

Ni vizuri zaidi pia ukimtumia fundi kukufanyia dizaini ya namna ya kutumia kona yako kulingana na kitu utakachoona kitaipendezesha zaidi.

# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO...

UMAARUFU WA MWIZI, HATMA YA KIFO CHAKE...

# Kinu cha nyuklia chapigwa, Russia, Ukraine zalaumiana

**KYIV,** UKRAINE

RAIS wa Ukraine Volodymyr Zelensky, ametaka vikwazo viwekwe dhidi ya sekta ya nyuklia ya Russia, kufuatia mashambulizi ya makombora dhidi ya kinu cha nyuklia cha Zaporizhzhya nchini Ukraine.

Katika hotuba yake ya kila siku ya juzi, Rais Zelensky alisema yeyote anayeleta vitisho vya nyuklia kwa watu wengine ni dhahiri hayuko katika nafasi ya kutumia teknolojia ya nyuklia salama.

Alitoa wito wa kuchukuliwa hatua za adhabu dhidi ya mamlaka ya nishati ya nyuklia ya Russia.

Ukraine na Russia zilishtumiana kwa mashambulizi dhidi ya kiwanda kikubwa zaidi cha nishati ya nyuklia barani Ulaya katika mji unaokaliwa na Russia wa Enerhodar. Ukraine imevishtumu vikosi vya Russia kwa kushambulia eneo hilo katika kile ilichokiita kitendo cha ugaidi.

Kwa upande mwingine, Wizara ya Ulinzi ya Russia, imewalaumu wanajeshi wa Ukraine kwa mashambulizi ya makombora na kusema moto uliokuwa ukiwaka katika kiwanda hicho umezimwa.

Hata hivyo, moja ya mitambo ya kiwanda hicho ililazimika kufungwa.

Siku chache zilizopita, Shirika la Kimataifa la Nishati ya Atomiki lilielezea wasiwasi wake kuhusu usalama wa kiwanda hicho cha kuzalisha umeme na kusema kuwa ukaguzi wa kiufundi ulihitajika haraka.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Ukraine ilitoa wito kwa jamii ya kimataifa kushirikiana na Russia kurudisha udhibiti wa kiwanda hicho kwa mamlaka ya Ukraine, ikionya kuwa ikiwa kinu kinachotumika kitashambuliwa, matokeo yanaweza kuwa mabaya.

Meya wa jiji la Enerhodar, Dmytro Orlov, aliwaonya watu waliosalia katika jiji hilo kwamba maeneo ya makazi yalikuwa yakishambuliwa kwa makombora kutoka eneo hilo la kiwanda cha umeme.

Katika ripoti ya kijasusi iliyochapishwa Ijumaa, Wizara ya Ulinzi ya Uingereza pia ilisema kuwa vikosi vya Russia vina uwezekano wa kuhatarisha ulinzi na usalama katika kiwanda hicho cha umeme .

Ripoti hiyo imeendelea kusema kuwa kufuatia miezi mitano ya uvamizi, nia ya Russia kuhusu kiwanda cha Zaporizhzhya bado haijabainika.

Ilieleza kuwa hatua hiyo inawezekana kudhoofisha usalama wa uendeshaji wake.

Marekani yatoa onyo kwa Afrika

BALOZI wa Marekani katika Umoja wa Mataifa, Linda Thomas-Greenfield, amezionya nchi za Afrika kutonunua bidhaa yoyote kutoka Russia,akitishia kuziwekea vikwazo kama zitafanya hivyo.

Linda wakati alipofanya ziara nchini Uganda, alisema bidhaa zitakazoruhusiwa kuingia katika bara hilo kutoka Russia ni nafaka na mbolea pekee. "Russia ina mtazamo kwamba vikwazo dhidi ya bidhaa za chakula na kilimo vimepelekea ongezeko la bei ambalo nchi zinakabiliana nalo. Ninataka kusema kwamba hatuna vikwazo kwa bidhaa zote za kilimo kutoka nchini humo," alisema Linda.

Alisema Russia inaweza kuuza nje bidhaa za kilimo, na chi nyingine zinaweza kuzinunua, ikiwa ni pamoja na mbolea na ngano. "Kwa mfano kuhusu mafuta, iwapo nchi itaamua kushirikiana na Russia katika maeneo ambayo yamewekewa vikwazo, basi zitakuwa zimekiuka vikwazo, na katika baadhi ya matukio pia itakuwa imekiuka vikwazo vya Umoja wa Mataifa. Na tunaonya nchi zisikiuke vikwazo ." alisistiza balozi huyo.

Nchi nyingi za Afrika zimeegemea katika mfungamano wa kutoegemea upande wowote katika vita vya Ukraine na Urusi.

Sababu kubwa ya kuwa katika mtazamo huo ni kutokana uhusiano uliopo baina ya Afrika na nchi za Magharibi ambazo nyingi ni wakoloni wa zamani wa mataifa ya Afrika, na wakati huo huo wasomi wengi wa Afrika waliosomea Russia wasingependa kujihusisha na vita hivyo.

**DW**

# Watu 11 wauwawa Ukanda wa Gaza

**GAZA,** PALESTINA

JESHI la Israel limefanya mashambulizi ya anga na kuyalenga maeneo ya wapiganaji katika ukanda wa Gaza mapema jana na kusababisha vifo vya watu 11, akiwamo msichana wa miaka mitano.

Tukio hilo lilisababisha wapalestina kurusha msururu wa makombora kuelekea kusini mwa Israel.

Mapigano hayo yanaweza kuwa vita kamili, yalianza juzi Ijumaa baada ya Israel kumuua kamanda mkuu wa wanajihadi wa Palestina.

Hata hivyo watawala wa kundi la Hamas katika maeneo hayo, walionekana kutojihusisha kwa sasa na mzozo huo, jambo ambalo kwa kiasi fulani limepelekea mzozo huo kutotanuka zaidi.

Mjumbe maalum wa Umoja wa Mataifa katika eneo hilo, Tor Wennesland, alitoa wito kwa pande zote kusitisha mara moja mapambano.

Katika kipindi cha miaka 15 iliyopita, Israel na Hamas wamepigana vita vikuu vinne na mapambano mengine kadhaa yaliyosababisha maafa kwa watu milioni mbili wa Palestina

**DW.**



Mgombea wa nafasi ya Urais kupitia Azimio la Umoja, Raila Odinga, akiingia eneo la Kibera jijini Nairobi kuomba kura kabla ya kuelekea katika uwanja wa Kasarani kumalizia kampeni yake jana: **PICHA: MTANDAO**

# Wakenya kuamua nani kuwa rais

**NAIROBI,** KENYA

WANANCHI wa Kenya wanatarajia kuingia katika vyumba vya kupigia kura keshokutwa baada ya kampeni kukamilika jana jioni.

Kampeni za urais nchini zilimalizika huku wagombea wakuu wawili wakihitimisha kwa mikutano mikubwa katika jiji la Nairobi.

William Ruto alimaliza kampeni zake katika uwanja wa Nyayo, wakati mpinzani wake Raila Odinga alikuwa uwanja wa Kasarani jijini humo.

Takriban wapiga kura milioni 22.1 watamchagua mrithi wa rais Uhuru Kenyatta, aliyeingia madarakani mwaka 2013 na ambaye hawezi kuwania muhula wa tatu kwa mujibu wa katiba ya nchi hiyo.

Kenya yenye makabila 46, inakabiliwa na mfumuko wa bei na hofu ya kujirudia ghasia za baada ya uchaguzi.

Mwaka 2007 hadi 2008, zaidi ya watu 1,100 walipoteza maisha katika vurugu za kisiasa na kikabila huku maelfu ya wengine wakilazimika kuyahama makazi yao.

Katika uchaguzi huu, polisi 150,000 watatawanywa nchini kote kwa ajili ya kuhakikisha kuna usalama

**DW**

MAKALA

# AFYA INAPOGEUKA KUWA BIASHARA



Na Magabilo Masambu - 0689157789

LEO katika safu hii tuzungumze kidogo kuhusu suala la afya nchini. Katiba ya Tanzania Ibara ya 8(1) (b) inaweka wazi lengo kuu la serikali. Inasema "lengo kuu la serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi" Lakini ibara 8(1) (c) inaongeza kwamba "serikali itawajibika kwa wananchi"

Kuna maswali kadhaa tunaweza kujiuliza. Mosi, kwa nini serikali ipo? Hilo limejibiwa hapo juu kwa mujibu wa Katiba.

Kwa nini wananchi wanalipa kodi? Wanalipa kodi ili wapate huduma bora kutokana kodi zao. Je zinazotolewa ni huduma au ni biashara? Hapa kila mtu atakuwa na jibu lake.

Nayazungumza haya kwa sababu moja. Kuna mambo nayaona kama serikali haitakuwa macho katika sekta ya afya, wananchi wataingia katika maumivu makubwa. Bahati mbaya sana serikali imekuwa na utamaduni wa kutazama zaidi taasisi zake kuliko kutupia macho hata taasisi binafsi.

Jambo la kwanza ni suala la wagonjwa kulazimishwa kula chakula cha hospitali. Kwanza, mgonjwa kula chakula ni jambo jema katika kuimarisha afya yake anapokuwa anaendelea na matibabu au baada ya tiba. Lakini kulazimishwa huku kumekaa katika mtindo wa biashara zaidi kuliko kujali afya ya mgonjwa.

Kuna baadhi ya hospitali hasa za binafsi zinawalazimisha wagonjwa kula chakula cha gharama kubwa sana ambacho hakiendani kabisa na gharama halisi. Mathalani, mgonjwa analetewa wali na maharage sahani inauzwa Sh. 10,000. Analetewa bakuli mbili za mtori au vikombe viwili vya uji gharama zile zile. Mgonjwa kwa siku anatumia Sh. 30,000 hadi 40,000.

Kibaya zaidi kuna wakati mgonjwa hajisikii kula chakula kinachoandaliwa siku hiyo lakini hospitali wanasema hakuna kingine ndicho hicho hicho! Unajiuliza hivi hapa tuko gerezani au hospitalini? Ukilazimisha kwamba ungehitaji chakula kingine unaambiwa hospitali ina mgahawa, lakini kile kilicholetwa utakilipia hata kama hutakula, kwa hiyo unalazimika kuingia gaharama mara mbili.

Nilimwuliza mhudumu mmoja katika hospitali fulani kwa nini wanalazimisha wagonjwa kula chakula tena kwa gharama kubwa? Akasema tunalinda afya za wgonjwa. Nikamuuliza kwa hiyo ndugu walioamua kumleta mgonjwa wao hospitalini ni hatari zaidi na kwamba wanaweza kumdhuru kwa chakula cha sumu kama wangetaka kufanya hivyo wangemleta hospitalini?

Baada ya swali hilo akabadilisha gia angani akasema tunafanya hivyo ili pasiwapo na tofauti ya vyakula.

Nikamwambia ni sawa lakini nikamwuliza wagonjwa wote wanafaa kula chakula cha aina moja, yaani aliyefanyiwa upasuaji na anayeumwa mguu? Jibu alilonipa ni: "Aah unajua huu ni utaratibu wa hospitali."

Nikamwuliza tena mbona gharama zinafanana kwa kila kinacholetwa halafu ni bei kubwa? Akasema mimi si msemaji!

Nachotaka kusema hapa ni kwamba tulinde uhai wa wagonjwa kwa kuwapunguzia mawazo wawapo hospitalini kwa sababu kuna uwezekano wengine wanachelewa kupona au kupoteza maisha kabisa kwa kuwaza gharama za matibabu pamoja na vyakula. Jambo la kuandaa chakula ni jema lakini gharama ziwe halisi na kama mgonjwa hajisikii kula chakula hicho, asilazimishwe kukilipia wakati hakula.

Suala la afya linapaswa kuwa huduma. Hatuwezi kusema iwe huduma moja kwa moja lakini kuwe na gharama za uchangiaji na si biashara. Wananchi wasio watumishi wa umma tunajua kazi kubwa wanayoifanya katika kulipa kodi nchini lakini wanapougua kwa sababu hawana bima ya afya, wananunua afya zao kwa gharama kubwa sana. Kulala tu hospitali unaambiwa kama una bima kitanda Sh. 20,000. Sasa wasio na bima bima hali yao inakuwaje?

Tufike mahali ambapo huduma za afya katika hospitali za umma na binafsi ziwe sawa ili mtu aamuwe aende wapi.

Ikiwezekana huduma katika hospitali za umma ziboreshwe zaidi maana cha kushangaza ni kwamba hata wenye dhamana ya kuzisimamia nao hawatibiwi humo.

Limekuwa kama jambo la shule tunajenga lakini watoto wetu wanasoma shule za binafsi. Maana yake wanaoshindwa kulipia gharama binafsi wafe!

Nishauri pawapo na chombo maalum, kama hakipo, cha kuchunguza mwenendo wa gharama za matibabu kama ilivyo Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) barabarani. Isiwe tu mtu anajiamulia kwa sababu hospitali ni yake na anapanga gharama anazotaka na kwamba asiyeweza asije. Yafanyike makubaliano na serikali kwa masharti kwamba serikali imaipatia hospitali hiyo hiki na kile lakini gaharama zisizidi kiasi Fulani. Vinginevyo tunarudi kule kule wakati wa ukoloni ambako huduma zilitolewa kwa matabaka- mzungu, mhindi na mwafrika. Tumepinga ubaguzi kisha tukaurudisha wenyewe.

Mwisho ni kuhusu rufani. Kuna baadhi ya hospitali zinanang'ang'ania wagonjwa hata baada ya kuonekana mmeshindwa kuwatibu.

Huu utaratibu unapoteza maisha ya Watanzania wengi sana. Kama mgonjwa kashindikana apewe rufani kwenda sehemu nyingine na kwa kufanya hivyo, hautakuwa udhaifu wa madaktari na hospitali kwa ujumla.

Suala la rufani, kwa mtazamo wangu, ni jambo la kawaida la kitabibu na si kwamba kufanya hivyo ni kushindwa na kwamba ni aibu. Mbona wengine wanawatibu na wanapona? Hivi madaktari walipokuwa shuleni hawakuwa wanasoma 'tuition' kwa mwalimu mmoja? Tena wanasema kabisa yule mwalimu namuelewa zaidi kuliko huyu. Kwa nini mkishakuwa madaktari hamwamini kwamba wengine wanaweza kutibu tatizo fulani ambalo kwa bahati mbaya mmeshindwa kulitatua kwa haraka?

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
ARUSHA-TANZANIA

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Tukuyu Stars, Mecco zilivyotikisa vigogo vya soka mpaka vikaomba po



Na Adam Fungamwango

MBEYA ni moja kati ya mikoa michache ambayo timu za Ligi Kuu ya soka zimekuwa zikitoa ushindani mkali kwa timu za Dar es Salaam, hasa zile kongwe za Simba na Yanga.

Inaungana na mikoa ya Morogoro, Tanga, Mwanza na Ruvuma ambayo timu zao zimefanikiwa kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara mbali na timu za Simba na Yanga.

Timu za mikoa hiyo zamani zilikuwa zikitwaa ubingwa wa Tanzania Bara au Ligi Kuu ya Muungano. Coastal Union ilitwaa Ubingwa wa Tanzania Bara mwaka 1988 lakini wapinzani wao, African Sports, mwaka huo huo wakatwaa ubingwa wa Muungano ambao ulikuwa ukizihusisha timu za Tanzania Bara na za Zanzibar.

Zamani bingwa wa Tanzania Bara anaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Afrika Mashariki na Kati, maarufu kama Kombe la Kagame kwa sasa lakini Ligi ya Mabingwa (zamani Klabu Bingwa Afrika) na Kombe la Shirikisho lilishirikisha timu ambazo zimeshinda nafasi ya kwanza na ya pili Ligi Kuu ya Muungano.

Timu zingine nje ya Dar es Salaam kutwaa ubingwa wa Bara au Muungano ni Mseto ya Morogoro, Pamba mwaka 1990, Majimaji ya Ruvuma 1998, Prisons ya Mbeya 1999, Tukuyu Stars ya Mbeya 1986, Mtibwa Sugar 1999 na 2000.

Leo tuziangalie timu za mkoa wa Mbeya ambazo zilitokea kuvuma kuanzia mwaka 1986 hadi 1991. Achilia mbali Mbeya City ambayo ilitinga Ligi Kuu Tanzania Bara na kucheza kuanzia msimu wa 2013/14, ikishangaza wengi kwa kutoa upinzani mkali mpaka kumaliza ikiwa kwenye nafasi ya tatu chini ya Azam iliyotwaa ubingwa na Yanga iliyomaliza nafasi ya pili.

Wengi walikuwa hawajui kuwa kuna timu ya Mbeya iliitwa Tukuyu Stars, si tu kwamba ilipanda na kucheza Ligi Kuu mwaka 1986 lakini ikatwaa ubingwa wa Tanzania Bara mwaka huo huo.

Ilikuwa kwa mara ya kwanza timu kupanda Ligi Kuu na kwenda kutwaa ubingwa. Haikuwa masihara. Ilikuwa timu iliyokamilika haswa.

Mwaka 1985 ikiwa daraja la pili, kwa sababu wakati huo Ligi Kuu ilijulikana kama Ligi Daraja la Kwanza, Tukuyu Stars hadi inaondoka Shinyanga kwa lori la mmiliki wa timu yao, Ramnik Patel 'Kaka' baada ya kushinda, haikuwa imejua kuwa imepanda daraja kutokana na kufungana kwa pointi na timu mojawapo katika kituo cha Shinyanga.

Walipata habari za kupanda daraja kupitia kipindi cha michezo cha Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD) wakiwa njiani maeneo ya Manyoni. Kwa furaha, mmiliki wa timu hiyo, aliendesha lori hilo la Isuzu kutoka Manyoni mkoani Singida hadi mjini Tukuyu.

Mwaka uliofuata, iliweka historia ya kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara na kuziacha klabu za Simba na Yanga zilizokuwa zikipokezana zikishangaa.

Timu hiyo iliundwa na wachezaji mahiri na ambao walitwaa ubingwa huo na wengine wakaja baadaye ambao ni Mbwana Makata, Kelvin Haule, Karabi Mrisho, Godwin Aswile, Ali Kimwaga, Selemani Mathew, Salum Kabunda 'Ninja', Abdallaah Mwela, Mohamed Kassanda, Michael Kidilu, Zacharia Siame, Hassan Sissu, Aston Pardon, Juma Rajab, Peter Mwakibibi, Justin Mtekere, John Alex, Sekilojo Chambua, Steven Mussa, Salum Kussi, Costa Magolosa, Joshua Kilale, Shaabn Katoto, Yohana Mjungu, Jimmy, Richard Lumumba, Yusuf Kamba, na Daniel Chundu.

Makocha wao kwa nyakati tofauti walikuwa ni Paul West Gwivaha na Athumani Juma Kalomba.

Kama kawaida, timu za Simba na Yanga ziliidhoofisha baada ya kugawana kwa kusajili asilimia kubwa ya wachezaji hao kwenye timu zao kabla ya kushuka daraja 1991.

Yanga ilizoa wachezaji wengi kama Kabunda, Mathew, Aswile, Alex, Mtekere, Makata baadaye Chambua, huku Simba ikiwachukua Kidilu, Aston na Haule, lakini pia baadaye iliwachukua Mathew na Aswile kutoka Yanga,

Misimu michache Mbeya ikaleta timu moja kabambe inaitwa Mecco. Ni timu iliyoleta kizaazaa kwani viongozi wa Simba na Yanga walikwenda kuishtaki Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) wakati huo Chama cha Soka Tanzania (FAT) kuwa wachezaji wake wanatumia dawa za kuongeza nguvu.

Ni kwa sababu walikuwa wana uwezo wa kucheza kwa muda mrefu bila kuchoka. Dakika za mwisho wao utafikiri ndiyo mpira unaanza.

Dakika 180 kwao ni ndogo sana. Walijinasibu wanaweza kucheza kwa dakika 300 bila kuchoka.

Rufani ya Simba na Yanga ambao waliamua kuungana, ilipigwa chini baada ya uchunguzi kudhihirisha kuwa wachezaji wa MECCO wanafanya sana mazoezi kwenye milima na kwa muda mrefu, ndiyo maana wako fiti. Simba na Yanga zilikuwa kwenye wakati mgumu zikicheza na Mecco, si Dar es Salaam au Mbeya.

Timu ambazo angalau zilikabiliana sawa sawa na MECCO zilikuwa Pamba ya Mwanza na Ushirika ya Moshi, zilizobaki ziliteseka sana.

Kikiso hicho kilichopanda daraja mwishoni mwa miaka ya 1980 na kushuka katikati ya miaka ya 1990, kiliundwa na wachezaji tishio kama George Mangula, Rashid Mandanje, Gabriel Mwitika, Mbaga Mwantinku, Charles Makwaza ambaye alikuwa nahodha, Danford Ngesi, Abeid Kasabalala, John Kanyiki, Betwel Africa, Ephraim Kayeta na Nassib Abbas.

# HADITHI

PRINCE Petit kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja mmoja tu na walipomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile, badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoena na mtu yeyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane tu alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani Anapofika umri wa miaka 25, baba yake mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi. Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

# Mwisho wa Mauaji-13

**Na Adam Fungamwangwo (0716 350534)**

HASNAT yeye aliacha kumuangalia mvamizi, badala yake akawa anamuangalia usoni mama yake.

Aliingiza mkono mfukoni na kutoa kibunda cha noti za shilingi elfu kumi kumi. "Jina lako Hasnat vilee eee."

"Ndiyo" Akajibu kwa sauti ndogo.

"Chukua hizi. Ni shilingi laki mbili. Ni zako. Utakwenda kununua nguo. Ila siyo kesho, kesho nataka uwepo hapa nyumbani." Wakati huo tayari binti alikuwa amenyanyuka na kuzichukua, akarudi tena kutaka kukaa chini alipokuwa amekaa mwanzo.

"Hapana, kaa hapa." Safari hii akamtaka kukaa kwenye kochi upande wake wa kulia, huku kushoto akiwa Hidaya.

"Haya mama na wewe zako hizi, ni laki tatu, laki mbili za kwako, moja ni kwa ajili ya chakula. Na kesho mimi nakuja hapa asubuhi, chai, chakula cha mchana na usiku nitakula hapa hapa. Na huenda nikaanza kula chakula hapa kuanzia kesho."

Tangu kuzaliwa hawakuwahi kushika pesa nyingi kiasi hicho. Mgeni katili aliyetaka kuwaua, akageuka kuwa neema kwao. Kwa pesa hiyo wao ni kama kulala masikini na kuamka tajiri. Kwa asilimia kadhaa wakaanza kumuamini.

Ilikuwa imeshatimu saa sita unusu usiku, Prince akawaaga kwa ahadi ya kufika tena kesho yake.

"Hata kama hamtaniamini kwa asilimia mia, sitarajii kama mtakwenda kuripoti polisi. Hata kama mtakwenda nitajua na hawatonikamata kwa sababu hakuna ushahidi. Na sitowafanya chochote tena. Niko tayari kukamatwa kwa sababu ya Hasnat. Kesho nitakuja hapa asubuhi tuyajenge mama."

"Sawa mwanangu, tunashukuru sana kwa kutuacha hai, pia kwa kutusaidia pesa hizi..."

"Hakuna haja ya kushukuru, mimi nilitakiwa niwaombe msamaha nyinyi. Poleni sana, laleni unono, tutaonana kesho. Hasnat baiii..." Akachukua bastola yake, akawaambia hawezi kuondoka mpaka ahakikishe wamefunga milango yote miwili kwa ajili ya usalama kwa sababu yeye amepata nafasi ya kuingia kutokana na udhaifu huo. Wakafanya hivyo.




**"Hakuna haja ya kushukuru, mimi nilitakiwa niwaombe msamaha nyinyi. Poleni sana, laleni unono, tutaonana kesho. Hasnat baiii..." Akachukua bastola yake, akawaambia hawezi kuondoka mpaka ahakikishe wamefunga milango yote miwili kwa ajili ya usalama kwa sababu yeye amepata nafasi ya kuingia kutokana na udhaifu huo.**

************************************

"Umemaliza kazi?

"Ndiyo baba." Akajibu kwa sauti ya chini, akijua kabisa hajatekeleza.

"Vizuri kabisa, sasa umekua mwanangu. Kila kitu kiko sawa. Ila kuanzia sasa hivi usifanye hivyo tena, nilikwambia ufanye hivyo kwa ajili ya kulipiza kisasi cha mama yako sawa?"

"Sawa Baba."

"Sasa urudi maisha ya kawaida. Uanze kujichanganya na jamii, kwa sababu wale waliokuwa hatari kwetu tumewamaliza.

"Ndiyo baba."

"Haya, mimi nakwenda kwenye mishughuliko yangu, sawa. Nitarudi jioni."

"Sawa baba na mimi jioni nitatoka kidogo, nataka niende nikasakate rhumba kidogo."

"Mmmh, mwanangu mara hii umeshaanza kuchangamka, ushakuwa mpenzi wa muziki?"

"Kazi ilikuwa ngumu baba, lakini nimeimaliza."

"Ila usiingie kwenye mtego wa polisi?"

"Hakuna hata sehemu moja baba ambayo nimeacha alama au ushahidi unaoweza kuwapa nafasi hao jamaa."

"Vizuri, Prince baadaye."

Dakika kumi tu baada ya mzee Pokwa kutoka, Prince naye aliwasha gari yake na kuondoka.

Ilikuwa ni tatu na nusu. Kwa mwendo wa gari lake Toyota IST, alijua kutoka Kinondoni Moscow hadi Mwananyamala Kisiwani mpaka saa nne na ushee atakuwa ameshafika.

Njiani alikuwa akimuwaza Hasnat. Binti ambaye ameonekana kubadilisha msimamo wake na maisha yake ghafla. Alimpenda kutoka moyoni. Alikuwa radhi apoteze kila kitu, lakini siyo kumpoteza msichana huyo kwenye maisha yake yaliyobaki.

Ilikuwa ni saa nne na dakika kumi alipofunga breki nje ya nyumba ya Hidaya. Akatabasamu. Ni kwa sababu aliimuona Hasnat akitokea dukani, akiwa amebeba mfuko.

Akafungua mlango taratibu na kushuka kwa madaha. Hasnat hakujua lolote. Siku alikwenda kutaka kufanya mauaji, gari aliliacha eneo la kuegeshea na kulazia magari, CCM Mwinjuma, Mwananyamala. Leo aliamua kwenda nalo kwa sababu alikwenda kwa furaha na amani.

"Kuna mzigo mwingine kwenye gari." Akasema ili sauti imfikie Hasnat aliyekuwa amefika karibu yake, lakini hakuwa akimwangalia. Akashtuka na uso wake akaugeuza kwa mtu yule aliyeshika mlango wa gari na kutaka kuufunga.

Akili yake ikafanya kazi haraka sana, kijana yule aliwahi kumuona wapi. "Hasnat nimefika mgeni wako." Maneno hayo ndiyo yaliyomshtua na kugundua kuwa alikuwa ni yule mgeni wao wa jana ambaye hata jina lake hawakulijua.

"He, kumbe wewe, umefika, yaani nilikuwa mbali sana." Akajibu akiwa amesimama karibu naye, jambo ambalo lilimfariji na kumpeleka mbali Prince.

"Yaani jana tu umeanza kunisahau Hasnat?" Akauliza kwa utani.

"Mmh, mwenzangu ulivyokuja jana siyo kama leo. Angalia leo ulivyotokelezea, na ndevu zako zile za jana umenyoa." Akajibu Hasnat kwa sauti ya chini ili asisikie mtu, lakini ikiwa laini kama sufi.

Prince aliangua kicheko. "Nimesema kuna mzigo mwingine humu ndani ya gari, ngoja nikupe kabisa uwe na mizigo miwili. Akatoa mfuko ambao ulikuwa na nyama, samaki, sukari na mafuta ya kupikia ambayo yalikuwa nyumbani kwao anakoishi na baba yake.

"Huo wako, lete nikusaidie mimi." Wakaingia kwenye mlango mkubwa wa bati. Hidaya alikuwa amekaa kwenye kizingiti cha nyumba "Karibuni." Akanyanyuka na kwenda kumpokea Prince mzigo, huku akimuacha Hasnat akiwa na mzigo wake wakaingia ndani.

"Karibu mwanangu." Akakaribisha tena.

"Ahsante mama." Akaitikia baada ya kukaa kwenye kochi. Sehemu ni ile ile ambayo alikaa jana usiku.

Hidaya na binti yake walishangazwa na mgeni wao alivyokuja leo ni tofauti na jana usiku. Walikuwa kama watu wawili tofauti. Wa jana aliingia akiwa mbabe, katili aliyejaa vitisho, ingawa baadaye akawa mpole ghafla.

Huyu wa leo ni mstaarabu

ITAENDELEA JUMAPILI



# Avril awasuta wanaomchimbua

MSANII wa muziki kutoka Kenya, Avril amezidi kusisitiza kwamba urafiki wake na Diamond Platnumz, sio wa kimapenzi na wanaofikiria hivyo hawawezi kuwabadilisha.

Avril amesema urafiki wake na Diamond una ubora maradufu na kwamba huwa hawaongei mara kwa mara na inapotokea basi inakuwa ni muhimu.

Fununu za wawili hao kutoka kimapenzi zilianza mwaka 2012, baada ya mrembo huyo kushiriki kwenye video ya wimbo wa 'Kesho' wa Diamond.

# Nandy hana ugomvi na Zuchu

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Nandy (picha kubwa chini), amesema yeye na msanii mwenzake Zuchu wanaongea vizuri na mara nyingi wanatumia mtandao wa Whassap kuwasiliana kwa kutumiana ujumbe.

Akizungumza na chombo kimoja cha habari alisema kuna watu wanataka kuwagombanisha kwa kuwalisha maneno, lakini anatumia busara kuzungumza na Zuchu kumueleza hajafanya jambo lolote baya.

"Watu wanaweza kuona yale yanayoendelea kwenye mitandao kuwa hatuongei vizuri, lakini ukweli sisi hatuna ugomvi tunazungumza na kuelezana mambo mengi lakini si vyema kuyaweka wazi kwa kila mtu," alisema Nandy.



Alisema kutokana na jina lake kutumika kibiashara mara nyingi anajiepusha na migogoro ambayo inaweza kumpoteza, jambo ambalo watu wanajitahidi kumpeleka huko kwa kumtungia uongo.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ALONSO AKARIBIA BARCA

KLABU ya Barcelona ipo katika mazungumzo na Chelsea kuhusu beki wa kushoto wa Hispania, Marcos Alonso, 31, na wana uhakika wa kufikia makubaliano ya kumsajili mchezaji huyo. ***(90min)***

### ALONSO AWAAGA WENZAKE

MARCOS Alonso, 31, amewaaga wafanyakazi katika uwanja wa mazoezi wa Chelsea wa Cobham huku akitarajia kukamilisha uhamisho wake wikendi hii. ***(Mail)***

### WAN-BISSAKA SOKONI

KLABU ya Crystal Palace imeonyesha nia ya kumsajili tena beki wa pembeni wa Timu ya Taifa ya England, Aaron Wan-Bissaka, 24, kutoka Manchester United. ***(Sky Sports)***

### ONANA AGEUKA LULU

EVERTON inajiandaa kuishinda West Ham katika mbio za kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Amadou Onana, 20, kutoka Lille. ***(Mirror)***

### FOFANA KUVUNJA REKODI

CHELSEA huenda ikalazimika kuvunja rekodi ya ada ya uhamisho ya pauni milioni 80 kwa beki - inayoshikiliwa na Harry Maguire - ili kumsajili beki wa kati wa Ufaransa, Wesley Fofana, 21, kutoka Leicester City. ***(Telegraph)***

### UDOGIE AKARIBIA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inapanga kukamilisha dili na Udinese kumnunua beki wa Timu ya Taifa ya Italia, Destiny Udogie, 19, wiki ijayo. ***(Fabrizio Romano)***

### KALIMUENDO AWINDWA

LEEDS United inalenga kumsajili kwa pauni milioni 22 mshambuliaji wa Paris St-Germain, Arnaud Kalimuendo, 20. ***(Sun)***

### DE JONG : SIONDOKI

KIUNGO wa kati wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong, 25, yuko tayari kusalia na klabu hiyo ya Hispania kwa mshahara uliopunguzwa licha ya Chelsea na Manchester United kumtaka. ***(Sport)***

### SESKO SAFARI IMEIVA

MAZUNGUMZO "yamebakia wazi" kati ya Manchester United na Red Bull Salzburg kuhusu uwezekano wa kumnunua mshambuliaji wa Slovenia, Benjamin Sesko, 19. ***(Sky Sports)***


### RAPHINHA ALITAKIA CHELSEA

MMILIKI wa Leeds United, Andrea Radrizzani amesema Chelsea ilikubali ada ya pauni milioni 65 kumnunua Raphinha, 25, kabla ya "ushawishi wa Barcelona" kumfanya winga huyo kuchagua kujiunga na klabu hiyo ya Hispania. ***(The Athletic)***

### MESSI ATAKIWA BARCA

KIUNGO wa kati wa zamani wa Barcelona, Cesc Fabregas amemtaka fowadi wa Argentina, Lionel Messi, 35, kuondoka Paris St-Germain na kurejea Nou Camp. ***(Mirror)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ... AYA




# ARTETA AKARIBIA REKODI YA WENGER

**LONDON,** England

Ni baada ya kufikisha ushindi wa 50 katika Ligi Kuu England akiwa amecheza mechi...

MIKEL Arteta aliandikisha ushindi wake wa 50 katika Ligi Kuu England (EPL) kama kocha wa Arsenal wakati timu yake ilipoilaza Crystal Palace mabao 2-0 kwenye mechi ya kwanza ya ligi hiyo iliyochezwa juzi.

**Na hilo linamfanya kuwa kocha wa pili aliyeshinda mechi nyingi zaidi kwa haraka kwa kikosi cha washikabunduki hao kwa nusu karne.**

Arteta imemchukua mechi 98 za ligi kufikia hatua hii, na ni Arsenal Wenger pekee aliyeweza kufanya hivyo - ambapo alishinda mechi 50 kwa kasi zaidi katika michezo 94.

Rekodi inazungumza mengi juu ya kazi ambayo Arteta amefanya na anayoendelea kuifanya kwa Arsenal.

Raia huyo wa Hispania, alipewa jukumu la kusawazisha mambo na kuanza tena baada ya kuondoka kwa Unai Emery, ambaye mwenyewe alirithi hali ngumu kutoka kwa Wenger aliyestaafu.

Wenger alikumbana na hali kama hiyo alipowasili London Kaskazini kwa mara ya kwanza msimu mwaka 1996 na kwa haraka alianza kuleta mapinduzi katika klabu kwa njia nyingi zaidi kuliko uwanjani tu.

Ndani ya miaka miwili, Arsenal walikuwa wakisherehekea kutwaa taji la Ligi Kuu England na Kombe la FA mara mbili.

Arteta ana changamoto ngumu zaidi mikononi mwake kufikia kitu kama hicho kwa haraka sana kutokana na ubora mkubwa wa Manchester City na Liverpool, lakini rekodi yake ikilinganishwa na ya Wenger ni kiashirio tosha kikosi chake kinaelekea katika njia sahihi.

Inafaa pia kuzingatia tangu mchezo wa kwanza wa Arteta, Desemba mwaka 2019, ni Pep Guardiola (70) na Jurgen Klopp (64) pekee ndio wameshinda zaidi ya michezo yake 50 ya Ligi Kuu England.

Kuhusu maendeleo ya mwaka baada ya mwaka, Arsenal tayari wako katika hali nzuri zaidi kuliko ilivyokuwa wakati huu mwaka jana walipofungwa na Brentford na kuwa mwanzo mbaya zaidi wa msimu tangu mwaka 1950.

Akiwa na miaka 40, Arteta bado ni kocha mchanga na kuna hisia mradi huu ndio unaanza tu.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI

MACHESTER UTD
VERSUS
BRIGHTON

1 | 1.63
X | 3.67
2 | 5.15

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BENTEKE AMFUATA ROONEY MAREKANI




**WASHINGTON,** Marekani

KLABU ya D.C. United imemsajili, Christian Benteke, kutoka Crystal Palace kwa mkataba wa miaka miwili na chaguo la kuongeza la mwaka mmoja.

Timu hiyo ilimsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Ubelgiji saa chache kabla ya kufungwa kwa dirisha la uhamisho la Ligi Kuu Marekani (MLS).

Mkataba wake amesaini hadi mwaka 2024, na chaguo la kuongeza hadi mwaka 2025.

"Christian ni mchezaji wa juu ambaye amecheza kwa kiwango cha juu kwa muda mrefu," alisema Kocha Mkuu DC United, Wayne Rooney.

"Uzoefu wake na uwezo wake wa kufunga mabao na kuisaidia timu itakuwa muhimu sana. Inafurahisha kwa timu na mimi mwenyewe kumwingiza ndani na kucheza. Atafanya mabadiliko makubwa."

Benteke sasa anasimama kama mchezaji wa tatu na wa mwisho wa timu hiyo kusajiliwa msimu huu, akiungana na mshambuliaji wa kimataifa wa Ugiriki, Taxi Fountas na kiungo wa kimataifa wa Iceland ,Victor Palsson.



## Cucurella atua rasmi Chelsea

**LONDON,** England

CHELSEA imekamilisha usajili wa beki wa Timu ya Taifa ya Hispania, Marc Cucurella kutoka Brighton kwa ada ya pauni milioni 60.

Beki huyo wa kushoto mwenye umri wa miaka 24 ambaye alifunga bao moja katika mechi 38 katika msimu wake pekee akiwa na Brighton, amesaini mkataba wa miaka sita.

"Nina furaha sana. Ni fursa kubwa kwangu kujiunga na moja ya klabu bora duniani," alisema Cucurella.

"Nitajitahidi kuwa na furaha hapa na kusaidia timu."

Hii ni rekodi ya mauzo ya Brighton, ikivuka uhamisho wa Ben White wa pauni milioni 50 kwenda Arsenal msimu uliopita wa joto.

Mhitimu huyo wa akademi ya Barcelona, Cucurella amecheza mechi moja katika kikosi cha Hispania na kuichezea timu ya vijana chini ya umri wa miaka 23 iliyoshinda medali kwenye Michezo ya Olimpiki ya Tokyo mwaka 2020.

Mwezi uliopita Brighton ilikataa dau la pauni milioni 30 kutoka kwa mabingwa wa Ligi Kuu England, Manchester City kwa ajili ya Cucurella, ambaye aliwasilisha ombi la uhamisho baada ya klabu hiyo kuonyesha nia ya kumhitaji.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# MAYELE AAHIDI ATAENDELEA KUTETEMA LIGI KUU 2022/23

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Yanga, Fiston Mayele amesema ataendelea kutumia staili yake ya kutetema ambayo imempatia umaarufu katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano mbalimbali ya kimataifa watakayoshiriki.

**Mbali na hayo, straika huyo raia wa Kidemokrasia ya Congo (DRC), amekitaja kikosi chake bora cha msimu uliopita, akiwaweka wachezaji watatu wa timu pinzani ya Simba, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr', Henock Inonga na Pape Sakho.**

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Mayele alisema hatabadilisha staili hiyo kwa sababu hata wachezaji wakubwa duniani wamekuwa na aina moja ya ushangiliaji ya kudumu, iweje yeye abadilishe.

"Siwezi kubadilisha ushangiliaji kwa sababu Ronaldo ni mchezaji mkubwa tu, amekuwa akihama timu mbalimbali, anakwenda huku anatoka anakwenda kule, lakini aina yake ya ushangiliaji ni hiyo hiyo anahama nayo tu. Kila anakokwenda anashangilia vile vile, kwa nini mimi nibadilishe, acheni niteteme tu," alisema huku akicheka.

Kuhusu kikosi chake bora cha msimu uliopita, alikitaja kuwa ni Djigui Diarra kutoka Yanga, Djuma Shaaban, Bakari Mwamnyeto (Yanga), Zimbwe Jr, Inonga (Simba), Yannick Bangala na Khalid Aucho wote kutoka timu yake.

"Viungo wa mbele ni Feisal Salum wa Yanga na Pape Sakho wa Simba, pale mbele anasimama George Mpole na mimi mwenyewe," alimaliza Mayele huku kocha mkuu wa kikosi hicho akiwa ni Nasreddine Nabi.

Nyota huyo amemtaja Farid Mussa ni mchezaji anayemfurahisha sana akiwa kambini na kama hayupo, basi anamkumbuka sana.

"Ukimwangalia kama mpole hivi, lakini ana maneno yule mwone vile vile anachekesha sana," alisema straika huyo.

Yanga itafungua pazia la msimu mpya kwa kuwakaribisha Simba katika mechi ya Ngao ya Jamii itakayochezwa Agosti 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.



Shabiki wa Yanga akionekana mwenye furaha huku akiwa amejichora jina la golikipa chaguo la kwanza la timu hiyo kuhitimisha sherehe za Wiki ya Mwananchi iliyofanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. **PICHA: YANGA SC**

# *Tanesco, Jeshi zaendeleza ubabe*

**Na Hadija Mngwai**

TIMU ya Tanesco ya wanaume na Jeshi Stars wanawake zimeendelea kutamba katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa ya Wavu yanayoendelea kwenye Uwanja wa Ndani wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Tanesco ilianza vyema katika mchezo wa awali wa ufunguzi wa ligi hiyo kwa kuwafunga Chui seti 3-0 na juzi ilipata ushindi dhidi ya Faru kwa seti 3-0 ikiwa ni mwendelezo mzuri katika kuwania taji la mashindano hayo.

Jeshi Stars wanawake ilipata ushindi baada ya kuzifunga Magereza seti 3-0 juzi huku katika mchezo wake mwingine iliwachapa NHIF seti 3-0 katika mchezo uliochezwa jana.

Mechi nyingine zilizochezwa juzi ni pamoja na NHIF iliyoifunga Serengeti seti 3-0, Jeshi Stars ikaiduaza Kigamboni seti 3-0 huku Nyika ikijikuta inapoteza kwa Chui kwa seti 3-0 na Mipango wao walikubali kichapo cha seti 3-0 kutoka kwa HVC.

NHIF wanawake walipoteza 3-2 dhidi ya Mafinga Parish, Golden Wings iliichakaza UDSM seti 3-1 na mechi za jana asubuhi Star Girls waliifunga Golden Wings seti 3-0 huku Magereza wakipata ushindi wa seti 3-0 dhidi ya Mafinga.

Ligi hiyo itaendelea leo kwa kuzikutanisha timu za Jeshi Stars dhidi ya Mafinga Parish, Star Girls dhidi ya UDSM, Magereza dhidi ya NHIF na KIUT dhidi ya Golden Wings, kwa upande wa wanawake.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 07/08/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1472 | Kawasaki Frontale vs Yokohama F Marinos | 2.29 | 3.52 | 2.64 |
| 13:00 | 1903 | Sagan Tosu vs Jubilo Iwata | 1.68 | 3.58 | 4.41 |
| 13:00 | 4401 | Thespakusatsu vs JEF United Chiba | 3.58 | 2.89 | 2.11 |
| 13:00 | 5591 | Chungnam Asan vs Gwangju | 2.80 | 3.09 | 2.39 |
| 13:15 | 1402 | Groningen vs FC Volendam | 1.73 | 3.70 | 4.30 |
| 13:15 | 1954 | PEC Zwolle vs De Graafschap | 2.01 | 3.48 | 3.33 |
| 13:30 | 1714 | Daegu vs Incheon Utd | 2.03 | 3.24 | 3.34 |
| 13:30 | 3441 | Daejeon Citizen vs Busan I Park | 1.49 | 4.04 | 5.52 |
| 14:00 | 2125 | Toulouse vs Nice | 2.77 | 3.27 | 2.45 |
| 14:00 | 4318 | Ostersunds vs Landskrona Bois | 2.51 | 3.36 | 2.75 |
| 14:00 | 5432 | Hibernian vs Hearts | 2.66 | 3.11 | 2.66 |
| 14:30 | 3975 | Standard Liege vs Cercle Brugge | 2.64 | 3.29 | 2.54 |
| 15:00 | 5039 | Zalgiris Kaunas vs Vilniaus Riteriai | 1.98 | 3.05 | 3.73 |
| 15:00 | 5174 | Torpedo Moscow vs FK Khimki | 3.70 | 3.35 | 1.96 |
| 15:15 | 2038 | FC Zurich vs FC Sion | 1.80 | 3.72 | 3.98 |
| 15:30 | 1398 | NEC Nijmegen vs Twente | 3.05 | 3.35 | 2.21 |
| 15:30 | 4354 | Vitesse Arnhem vs Feyenoord | 3.60 | 3.75 | 1.87 |
| 16:00 | 1140 | Angers vs Nantes | 2.64 | 3.14 | 2.64 |
| 16:00 | 1173 | Sirius FK vs Malmo | 4.21 | 3.87 | 1.66 |
| 16:00 | 2681 | Kalmar vs AIK Football | 2.74 | 3.09 | 2.43 |
| 16:00 | 3010 | Lens vs Brest | 1.52 | 4.30 | 5.40 |
| 16:00 | 4684 | Lille vs AJ Auxerre | 1.72 | 3.78 | 4.34 |
| 16:00 | 4710 | Montpellier vs Troyes | 2.17 | 3.31 | 3.21 |
| 16:00 | 5513 | Manchester Utd vs Brighton | 1.63 | 3.67 | 5.15 |
| 16:00 | 5824 | TS Galaxy FC vs Amazulu | 2.93 | 2.84 | 2.59 |
| 16:00 | 5901 | Leicester vs Brentford | 1.96 | 3.56 | 3.46 |
| 16:30 | 5137 | Stuttgart vs RB Leipzig | 4.19 | 3.74 | 1.74 |
| 17:00 | 2423 | Dundee Utd vs Livingston | 2.39 | 3.07 | 3.02 |
| 17:00 | 3139 | Copenhagen vs Brondby | 1.57 | 4.03 | 5.24 |
| 17:00 | 3342 | Coventry vs Rotherham | 1.71 | 3.50 | 4.79 |
| 17:00 | 5937 | KAA Gent vs KVC Westerlo | 1.65 | 3.88 | 4.73 |
| 17:30 | 1095 | FC Basel vs BSC Young Boys | 2.97 | 3.63 | 2.16 |
| 17:30 | 4410 | FC Lugano vs FC Luzern | 2.22 | 3.47 | 2.97 |
| 17:45 | 4159 | AZ Alkmaar vs GO Ahead Eagles | 1.38 | 4.70 | 7.00 |
| 18:05 | 5975 | Rennes vs Lorient | 1.34 | 5.02 | 7.84 |
| 18:30 | 1059 | West Ham vs Manchester City | 6.87 | 4.64 | 1.39 |
| 18:30 | 1371 | SuperSport Utd vs Chippa Utd | 2.05 | 3.00 | 3.85 |
| 18:30 | 1753 | FC Koln vs Schalke 04 | 1.71 | 3.96 | 4.11 |
| 18:45 | 2381 | Venezia vs Ascoli | 1.97 | 3.47 | 3.57 |
| 19:00 | 1568 | Verona vs Bari | 1.63 | 3.82 | 5.03 |
| 21:45 | 2179 | Antalyaspor vs Galatasaray | 2.47 | 3.40 | 2.65 |
| 21:45 | 5057 | Marseille vs Reims | 1.56 | 3.92 | 5.63 |
| 22:00 | 3522 | El Ittihad Alexandria vs Al Ahly Cairo | 2.62 | 3.43 | 2.49 |
| 22:00 | 4398 | Lokomotiva Zagreb vs HNK Rijeka | 2.35 | 3.23 | 2.74 |
| 22:00 | 4553 | Cukaricki St vs Spartak Subotica | 1.52 | 3.87 | 5.48 |
| 22:00 | 5539 | Salernitana vs Parma | 1.74 | 3.63 | 4.43 |
| 22:15 | 1716 | Stjarnan vs Breidablik | 3.68 | 3.73 | 1.79 |
| 22:15 | 3432 | Monza vs Frosinone | 1.84 | 3.52 | 4.03 |
| 22:30 | 4296 | GD Chaves vs Vitoria Guimaraes | 2.77 | 3.22 | 2.48 |
| 22:30 | 4327 | Portimonense vs Boavista | 2.09 | 3.16 | 3.57 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



Arteta akaribia rekodi ya Wenger UKURASA 21



Mshambuliaji mpya wa Yanga, Stephane Aziz Ki, akitambulishwa rasmi katika kilele cha sherehe za Wiki ya Mwananchi iliyofanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. **PICHA: YANGA SC**

## Simba: Jipangeni vizuri

**Na Saada Akida**

KUELEKEA kilele cha Simba Day, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally amesema wamejindaa vizuri na tayari beki wao mpya, Mohammed Ouattara ameungana na wachezaji wenzake.

Ahmed alisema maandalizi ya Tamasha la Simba Day yamekamilika na wamejiandaa kuwatambulisha wachezaji wote ambao wamewasajili na watakaowatumia kuelekea msimu mpya.

Alisema tayari wageni wao St. George ya Ethiopia wameshawasili nchini na wanaamini watakuwa kipimo sahihi kwa nyota wao kuelekea mchezo wa Ngao ya Jamii utakaochezwa Agosti 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Kikosi kipo imara na wachezaji wote waliosajiliwa wako nchini akiwamo Ouattara ambaye alikuwa na ruhusa maalum, lakini pia kuna 'suprize', mashabiki wetu wanatakiwa kujitokeza ili kujionea," alisema Ahmed.

Naye kiungo wa Simba, Jonas Mkude amewataka mashabiki wa timu hiyo kufika kwa wingi uwanjani kushuhudia tamasha hilo kwa sababu wamewaandalia mambo mazuri.

"Wao wamekuwa na nguvu kubwa, nina imani bila wao tusingekuwa hapa, Chama na wachezaji wote kasoro wale wapya ambao bado hawajawafahamu wameandaa kitu kikubwa kwa ajili yao, tunawahakikishia msimu huu watafurahi," alisema Mkude.

# Yanga Afrika yafunika

## Lakini yaacha sintofahamu Manara kutambulisha wachezaji katika kilele cha...

**Na Waandishi Wetu**

WAKIONGOZWA na Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana, wanachama na mashabiki wa Yanga waliadhimisha msimu wa tatu wa Wiki ya Mwananchi kwa kufurika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na kushuhudia utambulisho wa wachezaji wao wapya wa msimu wa 2022/2023.

**Hata hivyo, sherehe hizo zilигeuka baada ya Mhamasishaji wa Yanga, Haji Manara, kujitokeza uwanjani hapo akiwa amesindikizwa na mabaunsa wanne hali ya kuwa Kamati ya Maadili ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), ilimkuta na hatia na kumhukumu kifungo cha miaka miwili kutojihusisha na mchezo huo na kulipa faini ya Sh. milioni 20.**

Manara, aliingia uwanjani hapo saa 11:36 jioni na moja kwa moja alikabidhiwa kipaza sauti na MC, Maulid Kitenge ili aendelee na majukumu aliyotayarishiwa na mabosi wake.

Kivutio kikubwa katika utambulisho wa wachezaji alikuwa ni kiungo mshambuliaji Stephane Aziz Ki, raia wa Burkina Faso aliyesajiliwa kutoka Asec Mimosas ya Ivory Coast huku pia Bernard Morrison alirejea akitokea kwa watani zao, akiomba msamaha lakini akisema sasa amefuzu baada ya kumaliza mafunzo kwa Wekundu wa Msimbazi.

Wachezaji 28 waliotambulishwa jana ni pamoja na Djigui Diarra, Bakari Mwamnyeto, Abutwalib Mshery, Erick Johora, Kibwana Shomari, David Brayson, Abdallah Shaibu 'Ninja', Ibrahim Bacca, Dickson Job, Feisal Salum, Zawadi Mauya, Denis Nkane, Yusuph Athumani, Crispin Ngushi, Djuma Shaaban, Khalid Aucho na Salum Aboubakar 'Sure Boy'.

Wachezaji wengine ni Jesus Moloko, Heritier Makambo, Dickson Ambundo, Lazarous Kambole, Joyce Lomalisa, Yannick Bangala, Farid Mussa, Gael Bigirimana, Fiston Mayele na Aziz Ki.

Mashabiki wa Yanga waliingia kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kuanzia saa 4:00 asubuhi wakiwa wamevalia jezi za klabu yao za rangi ya njano, kijani lakini nyeusi ikionekana kutawala zaidi.

Kilele cha sherehe hizo za Wiki ya Mwananchi zilipambwa na wasanii mbalimbali akiwamo Ruby, Msaga Sumu, Mario, Mim Mars, Madee, Sir Jay pamoja na bondia aliyejizolea umaarufu hivi karibuni, Karim Mandonga.

Viongozi waliohudhuria ni pamoja na aliyekuwa Mwenyekiti wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla, makamu wake, Frederick Mwakalebela, Ridhiwani Kikwete (Naibu Waziri wa Ardhi) na mwenyeji wao, Rais wa sasa wa Yanga, Hersi Said aliyeambatana na mdhamini wao, Mohammed Gharib maarufu kwa jina la GSM.

### YANGA PRINCESS YAUA

Timu ya soka ya wanawake, Yanga Princess iliwapa raha mashabiki wa klabu hiyo baada ya kuichapa Ilala Queens mabao 4-0 katika mechi ya kirafiki ya utangulizi kwa kutumia nyota wake wapya iliyowasajili.

Mabao ya Yanga Princess katika mchezo huo yalifungwa na Precious Christopher aliyetikisa nyavu za wapinzani wao mara mbili, Cecilia Amali na Wincat Kaari.

Saa 10:40 jioni, nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, aliwaongoza wachezaji wenzake wakifuatiwa na benchi la ufundi la timu hiyo linaloongozwa na Kocha Mkuu, Nesreddine Nabi, wakiwa wamevalia suti nyeusi kuingia uwanjani kuwasalimia mashabiki wao.

Utambulisho ulifuatia baada ya mapema mchana nyota wa umri chini ya miaka 20 wakiongozwa na kocha wao, Said Maulid (SMG), kuwasalimia mashabiki.

Katika hatua nyingine, baadhi ya mashabiki wa timu hiyo waliliambia gazeti hili sherehe za mwaka huu ni 'bab kubwa' na wanawapongeza viongozi wao kwa kufanikisha hilo.

Katibu Mkuu wa Tawi la Sunami lililopo Mwananyamala, Dar es Salaam, Hawa Ahmadi, alisema mwaka huu tamasha lao limekuwa bora na la kipekee tofauti na mwaka uliopita.

"Tamasha la mwaka huu limekuwa la kihistoria tofauti na mwaka jana, watu wamejitokeza kwa wingi tofauti na tulivyofikiria," alisema Hawa.

Naye shabiki wa timu hiyo kutoka Tabata, Kessy Swedy, alisema amefurahi kutimiza ndoto zake za kuhudhuria sherehe hizo ambazo zimevutia idadi kubwa ya wana Yanga.

"Ninaamini baada ya kumaliza kilele cha sherehe hizi, tunakwenda kuendelea na mipango kwa ajili ya mchezo wa Ngao ya Jamii utakaochezwa wiki ijayo," Swedy alisema.

Katika kukamilisha sherehe hizo, Yanga ikiikaribisha Vipers FC kutoka Uganda katika mechi ya kirafiki ya kimataifa.

***Imeandaliwa na Adam Fungamwango, Saada Akida na Shufaa Lyimo.***

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >